**MULAMULA** aanika corona ilivyoathiri mapato ya balozi
UKURASA 4



**WANAFUNZI** maelfu wachaguliwa kidato cha tano, vyuo kati
UKURASA 4





UKURASA 9


# Nipashe

Jumatano Juni 2, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580599

www.ippmedia.com

The ... ital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710




Joseph Butiku

# Butiku aona ukakasi wabunge CHADEMA

**AZUNGUMZIA** tume huru ya uchaguzi... *Endelea Uk. 2*




Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na wafanyabiashara baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika Soko Kuu la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## WABUNGE WAJITOSA SAKATA LA CHATO

UKURASA 2

# Ziara ya kwanza ya Samia vilio, vicheko

UKURASA 3

**MICHEZO** **GOMES, MKWASA VITA VYA KIBABE, BURUDANI** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikabidhi cheti kwa Meneja wa Uhusiano wa Jamii wa Mgodi wa Barrick North Mara, Gilbert Mworia (kushoto), kutokana na mchango wa kampuni hiyo, kufanikisha uzinduzi wa mwongozo wa uwekezaji wa Mkoa wa Mara, katika hafla iliyofanyika mjini Musoma juzi. Wapili kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Mara, Mhandisi Robert Gabriel. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Butiku aona ukakasi wabunge CHADEMA

**Na Salome Kitomari**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, amesema suala la wabunge wa Viti Maalum 19 wa CHADEMA linapaswa kutatuliwa kwa kuzingatia katiba, sheria na kanuni ili kumaliza malumbano yaliyopo.

Akihojiwa juzi kwenye kipindi cha Dakika 45 cha ITV, alisema ni muhimu suala la wabunge hao likaangaliwa kwa jicho la katiba, sheria na kanuni badala ya kuendelea na malumbano.

"Ni muhimu kuangalia nani amekosea na kukubali pale yule aliyekosea aseme amekosea, kama ni CHADEMA aseme nimekosea, Spika aseme amekosea, katika sheria au katiba na heshima ya utu wetu hakuna aibu kukosea katika sheria aibu ni kukataa hata sheria ikikwambia umekosea," alisema.

Alisema: "Kama mtu mzima hili jambo limekaa muda mrefu sijui kwanini, ni mvutano usiyo wa lazima, ni jambo la sheria litazamwe limalizike hakuna haja ya kuleta ugomvi au kama linakuzwa kisiasa kuonyeshana ubabe, lakini hiyo siyo siasa nzuri."

"Kama CHADEMA wanasema tumeshawafukuza siyo wanachama wetu, nani anabisha, na katika kuwafukuza amefuata utaratibu wa chama na aliwapa nafasi ya kujieleza kwanini walitenda alivyotenda na hawakustahili kufukuzwa."

"Kati yao yupo ambaye hafuati utaratibu...nililo na uhakika CHADEMA inasema ilishawafukuza, swali ni kama alifuata utaratibu, huko aliko bungeni wako kwa utaratibu wa sheria na katiba za nchi? Ni lazima kuzungumza ili kumaliza hilo."

Alisema kama waliofukuzwa ni wanachama wao na utaratibu huwezi kuingia bungeni bila chama, lakini bado wapo inazua maswali kama wako CHADEMA au CCM, na kwamba anaamini viongozi watalishughulikia.

Butiku alisema alichosikia ni CHADEMA kusema kuwa walishawafukuza wabunge hao, na kwa mujibu wa katiba huwezi kwenda bungeni bila chama.

"Lakini katika utaratibu Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imewatangaza ndiyo washindi. Mkifika hapo mnafanya nini, mnatafuta ukweli hakuna haja ya malumbano," alisema Butiku.

Butiku alisema nchi imekomaa ina miaka 60 sheria na katiba, na kwamba ni jambo la utaratibu na kwamba sheria haitarajiwi kuvunja katiba bali ndani ya mfumo.

"Vyama tunavyoanzisha lazima viwe ndani ya mfumo wa katiba ambayo ndiyo sheria mama. Ubishi huo utakuwa wa kikatiba au kisheria au kanuni za vyama," alisema.

TUME YA UCHAGUZI

Butiku alisema hoja iliyopo ni wajumbe wa Tume ya Usimamizi na Uchaguzi wanaoteuliwa na rais.

"Huwezi ukateuliwa na Rais kuwa NEC halafu Rais ni mwanachama wa chama kimoja na wewe amekuteua katika kutekeleza wajibu wako wa Tume usiache kumpendelea aliyekuteua, hii ni hoja ya ubinadamu," alisema na kuongeza;

"Lakini nchi hii inaongozwa kwa sheria na katiba Rais akikuteua lazima ufuate ya kwangu (Rais), ila ipo hisia kuwa ukiteuliwa na rais lazima upendelee upande wake, ila mimi nasema tukiendelea na hisia hizo hatutamwamini yeyote.

"Hata tukiteua tume ya kusimamia bado binadamu atakupendelea, katiba ipo, sheria na taratibu za kufuata, kama yupo mtu au Rais anakwambia usifuate, ondoka kwenye Tume hiyo ndiyo uwajibikaji," alisema.

Alitolea mfano akiwa mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba alipigiwa simu na baadhi ya viongozi wakubwa ambao walitaka kumpangia cha kufanya, lakini alikataa na kufuata utaratibu.

# Wabunge wajitosa Chato kuwa mkoa

**Na Romana Mallya**

BAADHI ya wabunge wamefunguka sakata la Chato kuwa mkoa, na kueleza kuwa wanaopinga watakuwa na mambo yao binafsi na kutaka wawaache wananchi wenyewe waamue.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe jana jijini Dodoma wabunge ambao mikoa yao inaguswa moja kwa moja kwenye suala hilo, walisema Chato itakapokuwa mkoa itawezesha kuanzishwa kwa huduma mbalimbali za kiuchumi, kijamii, biashara na miundombinu kujengwa.

Mbunge wa Biharamulo, Mhandisi Ezra Chiwelesa, alisema kuanzisha mkoa ni kusogeza huduma kwa wananchi kwa sababu hizo ni halmashauri zinazoungana.

Alisema licha ya baadhi ya madiwani kupinga, haimaanishi maeneo mengine wamekataa.

"Madiwani wa Chato wapo tayari kwa sababu hizo ni halmashauri zinazoungana, Geita wakipinga haimaanishi Biharamulo imekataa, Geita ikipinga haimaanishi Sengerema wamekataa, kwa mfano Bukombe, Chato wao wako tayari kukaa kwenye mkoa mpya," alisema.

Alisema kilichotokea Geita ni wilaya ina majimbo matatu ya uchaguzi, ambao wanakaa kwenye halmashauri moja, na kwamba kilichokuwa kinapingwa na madiwani wa Geita ni kuachia Busanda, lakini hawakupinga kuanzishwa mkoa.

"Suala la mkoa lilianza muda mrefu, kwa wenzangu wa Biharamulo, Ngara na Kakonko sidhani kama kuna mtu amepinga maana mwisho wa siku tunapoanzisha mkoa huduma zinasogea karibu na wananchi na huduma za kiuchumi, biashara na miundombinu itaanza kujengwa," alisema.

Alisema wanaopinga kuwa hawataki kuwe mkoa watakuwa na mambo yao binafsi na kuwataka waache wananchi wenyewe waamue.

"Tunachokiona ni kama kukuza mambo, binafsi sioni kama ni sahihi kwa sababu hili jambo lilikuwapo... sasa tunapoongelea suala la mkoa mpya halafu unaanza kusema mbona mkoa fulani haujagawanywa, shida kubwa ninayoiona hapo kama mbunge ni jina Chato, suala siyo mkoa, ndiyo maana wengine wanasema kama ndiyo hivyo makao makuu yasiwe Chato.

"Kuna watu wakisikia jina Chato wanateseka, hii ndiyo shida, suala la kuwa mkoa ni jambo zuri, lakini kuna mambo ya kisiasa yanaingizwa."

Kuhusu idadi ya watu, alisema wanapoongelea mkoa lazima wajadili idadi ya watu na kueleza mkoa unaoongoza kwa watu wengi ni Dar es Salaam, Mwanza na Kagera.

Alisema Geita kwa mujibu wa sensa iliyopita, una watu milioni mbili na kueleza kuwa huenda sasa idadi hiyo ikawa imeongezeka zaidi.

"Kigoma ambayo tunataka kuichukua milioni 2.7 ambapo inalingana na mkoa wa Morogoro, tunaposema tunasogeza huduma na kutokuwa mkoa imetuathiri nini, kuna vitu vingi haviwezi kufanyika, tunapopata fursa ya kwenda kuwa mkoa mpya tunapata fursa mbalimbali kama mkoa," alisema.

Mbunge wa Busanda, Tumaini Magessa, alisema utaratibu wao wa kufanya uamuzi hutumia vikao halali kwa kuanzia kamati ya fedha, kamati ya madiwani, kamati ya ushauri wa wilaya na mkoa.

Alisema vikao vyao kuhusu hoja hiyo wameshakaa na uamuzi umeshatoka ambao ndiyo mapendekezo ya mkoa, lakini hakuweza kuhudhuria kikao kwa sababu ya vikao vya bunge vinavyoendelea.

"Wananchi wa jimboni kwangu hawawezi kupingana na mambo ambayo nao wana maslahi nayo, sijasikia mahali popote kama kuna tatizo, kilichoamuliwa na mkoa ndiyo uamuzi wa wananchi kwa sababu kiliwasilishwa na wawakilishi wao," alisema.

Magessa alisema hajasikia watu wanaopinga zaidi anachojua ni michakato ya kisheria inaendelea hawawezi kwenda kwenye maoni ya mtu mmoja mmoja.

"Wanaopinga siyo wapingaji ni watu wanajisherehesha mtu akitaka kuzungumza anapaswa kuzungumza kwenye vikao halali anayeuzungumzia kwenye WhatsApp huyo anasherehesha," alisema.

Mbunge wa Sengerema, Tabasam Mwangao, alisema hawezi kuzungumza jambo ambalo halijapelekwa bungeni.

HABARI KITAIFA

# Ziara ya kwanza ya Samia vilio, vicheko

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan amefanya ziara ya kwanza tangu alipoapishwa Machi 19, mwaka huu kuongoza nchi, ambayo imeacha vilio na vicheko kwa baadhi ya watendaji na viongozi.

Rais Samia alifanya ziara ya kushtukiza katika maeneo mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam ikiwamo Soko Kuu la Kariakoo, Mradi wa Mabasi ya Mwendokasi eneo la Mbagala, pamoja na Hospitali ya Mwananyamala.

**KARIAKOO**

Akiwa katika Soko Kuu la Kariakoo, Rais Samia aliwasimamisha kazi viongozi wa soko hilo kwa muda usiojulikana ili kupisha uchunguzi, kwa sababu zilizotajwa kuwa ni usimamizi mbovu, mpangilio wa bidhaa usioridhisha na utozaji wa kodi kubwa.

Akiwa katika soko hilo, Rais Samia alieleza kuwa serikali imeamua kufanya tathmini ya uendeshwaji wa soko lote kwa kuwa hali aliyoikuta ndani na nje haikumridhisha, pia kufanyika kwa vitu vinavyonufaisha soko na siyo wafanyabiashara sambamba na mipango ya uingizwaji wa bidhaa usiompa nafuu mfanyabiashara mdogo.

Rais Samia alisema: "Maamuzi yangu ni kwamba tutafanya tena tathmini ya uendeshwaji wa soko na tuone kama linaendeshwe na uongozi uliopo au lichukuliwe na Jiji, pia nimeangalia vizuri humo ndani ni vurugu mechi, huoni bidhaa gani iko wapi, unakuta anayeuza vyerehani yupo katikati mwa anayeuza dawa za kilimo na mambo mengine."

Aliongeza: "Hivyo wakati serikali inafanya tathmini ya soko nimwagize Waziri wa TAMISEMI (Ummy Mwalimu) kuusimamisha kidogo uongozi uliopo na tutaangalia mpaka ngazi gani na vyombo vya seririkali vifanye uchunguzi kwanza halafu tutakuja kutoa maamuzi, kwa ujumala hali iliyoko hapa haikuniridhisha na tunakwenda kuchukua hatua zinazofaa."

Pia aliwataka wafanyabiashara kuendelea kufanya kazi zao kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa katika eneo hilo kwani kumekuwa na baadhi ya watu walioweka bidhaa zao kwenye njia ya watembea kwa miguu kinyume na taratibu.

**MWENDOKASI**

Akiwa eneo la Mbagala katika Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka ambao ujenzi wake unaendelea, Rais Samia alieleza kutoridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi huo kwakuwa unaenda tofauti na matarajio.

Alisema katika eneo la Mbagala kuna idadi kubwa ya watu ndiyo maana serikali iliamua kuupeleka mradi huo ili ukawasaidie katika suala la kupunguza adha ya usafiri, hivyo unavyo chelewa kukamilika unachangia kudorora kwa uchumi.

"Tunajua Mbagala watu ni wengi na sisi tumeamua kuwajengea huu mradi waende haraka na shughuli zao za uchumi, kwahiyo kila wanavyo tucheleweshа na uchumi wetu unazubaa, hivyo nimekuja kuangalia sababu zinazochelewesha kama ni upande wa serikali tuchukue hatua na kama ni mkandarasi naye tumchukulie hatua," alisema Samia na kuongeza:

"Mradi huu kwa sasa ulikuwa ufikie kama asilimia 60, lakini kwa taarifa nilizozipata leo 'jana' mradi huu umefikia asilimia 16 tu, pia tumeongea na makandarasi na wasimamizi wa mradi tumeona ni kitu gani kinachelewesha mradi, lakini kwa ujumla kama serikali hatujaridhishwa na mradi unavyoendeshwa."

Aliongeza: "Mkandarasi aongeze kasi ya ujenzi wa mradi huu, tunataka umalizike ili tuingie kwenye njia nyingine lakini kumalizika kwa mradi huu kutaiwezesha serikali au wananchi kuwarahisishia safari zao, na kwenda haraka kwa uchumi wetu".

**HOSPITALI MWANANYAMALA**

Rais Samia alisema alipata taarifa ya changamoto zinazoikabili Hospitali ya Mwananyamala ikiwamo uhaba wa wauguzi, dawa na magari ya kusafirishia wagonjwa na kuahidi kuwa serikali itazishughulikia.

Hivyo, alitoa msaada wa mashuka 200 na aliwataka wauguzi kufanya kazi kwa bidii wakati serikali ikishughulikia maslahi yao.

Rais Samia alisema: "Nimetoa zawadi ya mashuka 200, ili wagonjwa wetu wapate kulala pazuri sasa mkikuta mashuka yamechanika na wagonjwa wamelazwa hapana pigeni kelele tusikie kwa sababu idadi hiyo si haba, najua hali ni ngumu ila wamepata ya kubadilisha na vivyo hivyo tutakwenda katika hospitali zingine kurekebisha mambo."

Alisema: "Lingine ninakwenda kuangalia maslahi ya wauguzi jinsi uchumi utakavyoniruhusu basi nitawawekea vitu vizuri, lakini ili uchumi ukue tufanye kazi, wananchi wawe na afya wafanye kazi uchumi ukue tugawane wote." Aidha, Rais Samia alitoa wito kwa wananchi kwa ujumla kuchukua tahadhari za ugonjwa wa Covid-19.

# Jaji Imani Aboud achaguliwa Rais wa Mahakama ya Afrika

**Na Daniel Sabuni, ARUSHA**

JAJI Imani Aboud wa Mahakama Kuu ya Tanzania, amechaguliwa kuwa Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu.

Jaji Imani anakuwa mwanamke wa pili kuongoza mahakama hiyo na Mtanzania wa pili kushika wadhifa huo, tangu kuanzishwa kwake mwaka 2006.

Akitangaza jana matokeo hayo bila kutaja idadi ya kura zilizopigwa, Rais Mstaafu wa Mahakama hiyo, Slyvan Ore, raia wa Ivory Coast, alisema Jaji Aboud, amewashinda majaji wengine wanne wanawake kutoka Nigeria, Cameroon na Malawi.

**"Kwa ushindi huu, sasa Rais Iman Aboud atatuongoza kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia leo (jana). Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya kimataifa iliyoanzishwa na nchi za Afrika ili kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu na watu barani Afrika," alisema Ore.**

"Kwa ushindi huu, sasa Rais Iman Aboud atatuongoza kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia leo (jana). Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya kimataifa iliyoanzishwa na nchi za Afrika ili kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu na watu barani Afrika," alisema Ore.

Licha ya kutotangazwa idadi ya kura zilizopigwa, majaji walioshiriki uchaguzi huo wa kihistoria walikuwa 11.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa kuwa Rais wa Mahakama hiyo, Jaji Imani alisema:

"Kwa imani mliyoionyesha kwangu na nchi yangu naahidi kutekeleza majukumu ya urais kwa haki na usawa ili kuleta haki kwa binadamu waliopo mataifa yote ya Afrika."

Pia katika uchaguzi huo, Jaji Blaise Tchikaya wa Jamhuri ya Watu wa Congo, alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Mahakama hiyo.

Awali, Jaji Slyvan Ore, Rais aliyemaliza muda wake, alimshukuru Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kwa ushirikiano mkubwa ambao unafanikisha majukumu ya mahakama hiyo katika kuwezesha upatikanaji wa haki za binadamu katika Bara la Afrika na dunia.

Alizitaka nchi zilizoridhia kuanzishwa kwa mahakama hiyo, kutumia nafasi hiyo kutatua matatizo ili kuleta amani na utulivu na hatimaye haki za binadamu kushamiri katika maeneo yao.

"Haki za binadamu ni msingi mkubwa wa maendeleo, Waafrika watumie nafasi hiyo muhimu. Sio lazima wafike kwenye mahakama hiyo wanaweza kuleta malalamiko kwa njia ya mtandao na yakasikilizwa na kupatiwa ufumbuzi," alisema Rais huyo.



# Mulamula: Corona imeathiri mapato

**Na Romana Mallya**

MLIPUKO wa virusi vya corona umesababisha kupungua kwa mapato ya serikali katika majengo ya balozi za Tanzania kutokana na kukosa wapangaji.

Waziri wa Mambo ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2020/21, wizara ilipanga kukusanya Sh. bilioni 2.551 na kati yake, Sh. 47,170,000 ni makusanyo ya Makao Makuu ya wizara na Sh. bilioni 2.5 ni makusanyo kutoka balozi za Tanzania.

"Vyanzo vya mapato hayo ni uhakiki wa nyaraka, pango la majengo ya serikali nje ya nchi na mauzo ya nyaraka za zabuni.

"Katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Aprili 30, mwaka huu, wizara ilikusanya jumla ya Sh. milioni 756.182, sawa na asilimia 29.6 ya lengo lililopangwa kwa mwaka wa fedha 2020/21," alisema.

Waziri huyo alisema kupungua kwa mapato hayo kumetokana na kukosekana kwa wapangaji katika baadhi ya majengo ya serikali kwenye balozi za Tanzania kutokana na athari za uwapo wa janga la corona.

"Nchi nyingi duniani zilichukua hatua za kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huu kwa kufunga shughuli muhimu za kijamii na uzalishaji zilizosababisha kampuni na



ofisi nyingi kufungwa na kufanyia kazi zake kutokea nyumbani," alisema.

Vilevile, waziri huyo alibainisha mapato yatokanayo na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) yameshuka kwa sababu ya kupungua kwa mikutano.

Alisema kituo kimeendelea kuendesha biashara ya mikutano; upangishaji wa nyumba na ofisi; na kutoa huduma ya afya kupitia hospitali inayomilikiwa na kituo hicho.

Alisema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, kituo kilipanga kukusanya mapato ya Sh. bilioni 16 lakini hadi mwezi Aprili mwaka huu, kilikusanya mapato ya Sh. bilioni 7.97, sawa na asilimia 48 ya malengo.

"Mapato haya yalitokana na huduma za kumbi za mikutano (AICC na JNICC) Sh. 2,608,160,544 kati ya lengo la Sh. 6,339,350,000; upangishaji wa ofisi na nyumba za kuishi Sh. 2,995,497,441 kati ya lengo la Sh. 4,956,540,000; huduma za hospitali Sh. 2,366,982,510 kati ya lengo la Sh. 4,705,669,000," alisema.

Alisema sababu za kushuka kwa mapato ya kituo ni kupungua kwa idadi ya mikutano hali iliyochangiwa kwa kiasi kikubwa na kikwazo cha corona.

Alisema katika kipindi hicho kituo kilihudumia mikutano 143 ya kitaifa na minne ya kimataifa ambayo ilileta washiriki 46,811 wa kitaifa na 3,621 wa kimataifa.

Wizara hiyo inakadiria kutumia Sh. bilioni 192.2 katika mwaka ujao wa fedha. Kati yake Sh. bilioni 178.7 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 13.5 ni kwa ajili ya maendeleo.

***Soma hotuba ya Waziri Mulamula Uk. 9-16**

# PM atoa maagizo kuhusu mazingira

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imetoa maagizo kadhaa katika kuhakikisha mazingira yanatunzwa ikiwamo majengo ya serikali na binafsi kuzingatia ufungaji wa mifumo ya nishati ya gesi au matumizi mbadala kwa ajili ya matumizi ya kupikia.

Maagizo hayo yametolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, na kuelekeza taarifa ya utekelezaji wake aipate kila baada ya miezi sita.

Pia ameliagiza Jiji la Dodoma kuweka mpango mkakati wa maeneo yaliyopimwa na yatakayopimwa yaonyeshe eneo la kupanda miti kutokana na ripoti ya tatu ya Hali ya Mazingira nchini ya mwaka 2019, kuonyesha Jiji hilo ni miongoni mwa maeneo ambayo yamebainishwa kuwa ni kame na yana kasi kubwa ya ukataji wa miti.

Aliyasema hayo jijini hapa alipokuwa akitoa tamko la serikali la Maadhimisho ya Wiki ya Mazingira Duniani ambayo imeanza jana hadi Juni 5, mwaka huu.

"Wahandisi, wachora ramani, wajenzi wanaopewa kazi wahakikishe kwamba ramani inachorwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba lazima ihusishwe na mchoro wa eneo la kupeleka miundombinu ya gesi au matumizi ya mkaa mbadala badala ya kutumia jiko la kuni."

Majaliwa aliagiza teknolojia bora ya uzalishaji wa mkaa mbadala itunzwe na kusambazwa kote nchini ili wananchi wengi kutumia mkaa mbadala na kupunguza uharibifu.

"Wizara, taasisi na mashirika yote ya serikali pamoja na binafsi kutoka sekta binafsi na vikundi vya ujasiriamali wanaozalisha, wanaotumia nishati ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia au shughuli za uzalishaji sasa waanze kutumia nishati mbadala au mbadala wa mkaa," alisema. Pia aliagiza taasisi, shule, vyuo, hospitali na majengo makubwa yakiwamo ya serikali au binafsi ni lazima kuzingatia ufungaji wa mifumo ya nishati ya gesi kwa ajili ya matumizi ya kupikia.

# 148,000 wachaguliwa kidato cha tano, vyuoni

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WANAFUNZI 148,127 kati ya 153,464 wamekidhi vigezo na sifa za msingi za kujiunga na kidato cha tano na vyuo vya elimu ya ufundi kwa mwaka 2021.

Wakati wanafunzi hao wakipata nafasi hizo, serikali imesisitiza hakutakuwa na fursa ya kufanya mabadiliko yoyote ya shule kutokana na ukosefu wa nafasi kwenye shule husika.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alisema jana kuwa wanafunzi hao ni waliofanya mtihani wa kidato cha nne mwaka jana ambao walipata daraja la I - III.

Alisema katika matokeo hayo wanafunzi waliopata madaraja hayo walikuwa 153,464 wakijumuisha wasichana 67,135 na wavulana 86,329, sawa na asilimia 35.06 ya watahiniwa waliofanya mtihani.

"Waliochaguliwa ni wasichana 63,878 na wavulana 84,249, sawa asilimia 33.34 ya wanafunzi hao waliofanya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2020, pia imejumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalum 288," alisema.

Ummy alisema watahiniwa wa kujitegemea waliofanya mtihani wakiwa chini ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) waliofaulu kwa madaraja hayo ni 479 na waliochaguliwa 287.

Alisema wanafunzi hao waliochaguliwa ni kutoka shule za serikali, zisizo za serikali, watahiniwa wa kujitegemea na wanafunzi waliosoma nje ya nchi ambao matokeo yao yamefanyiwa ulinganifu na Baraza la Mitihani (NECTA).

Waziri huyo alisema kuwa kati ya hao waliochaguliwa, wanafunzi 87,663 watajiunga na kidato cha tano katika shule 476 za serikali ikiwamo shule mpya 42.

Alibainisha wanafunzi wa mahitaji maalum wote waliofaulu na kukidhi vigezo wamepangiwa kuendelea na elimu ya kidato cha tano.

Alisema wanafunzi 41,504, sawa na asilimia 47.34, watajiunga kusoma tahasusi za sayansi na hisabati huku wanafunzi 46,159, sawa na asilimia 52.66 wamechaguliwa kusoma tahasusi za masomo ya sanaa na biashara.

Kadhalika, alisema wanafunzi 1,598 wamechaguliwa kujiunga na fani mbalimbali katika vyuo vinne vya ufundi ambavyo ni Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Chuo cha Usimamizi wa Maendeleo ya Maji (WDMI) na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST).

Alisema wanafunzi 55,308 wamechaguliwa kujiunga kwenye kozi mbalimbali za ngazi ya astashahada na stashahada katika vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi vinavyosimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

"Wanafunzi 2,235 wamechaguliwa kujiunga na vyuo vya afya ngazi ya stashahada, wanafunzi 5,757 wamechaguliwa kujiunga na vyuo vya ualimu ngazi ya astashahada ya elimu maalum, awali, michezo, msingi na ualimu wa shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiingereza," alisema.

Ummy alisema wanafunzi 1,709 wamechaguliwa kujiunga na vyuo vya ualimu ngazi ya stashahada ya sayansi, hesabu na TEHAMA, na wanafunzi 45,607 wamechaguliwa kujiunga na vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi katika kada mbalimbali.

Alisema muhula wa kwanza kwa wanafunzi wa kidato cha tano utaanza Julai 5, mwaka huu.

"Hivyo, wanafunzi wote waliopangwa kujiunga na kidato cha tano kwa mwaka 2021 wanapaswa kuanza kuripoti katika shule zao kuanzia Julai 3, mwaka huu, siku ya mwisho ya kuripoti itakuwa Julai 18, mwaka huu," alisema.

Ummy alisema endapo mwanafunzi atachelewa kuripoti, nafasi yake itachukuliwa na mwanafunzi mwingine aliyekosa nafasi.

"Serikali ya Awamu ya Sita ingependa kuona wanafunzi wote waliochaguliwa kwenda kidato cha tano wanajiunga kwa pamoja ndani ya muda uliopangwa, hivyo serikali inawahimiza wanafunzi ambao wameshakata shauri kujiunga na shule za binafsi kuthibitisha kujiunga na shule hizo kupitia mfumo wa 'Selform' uliotumika wakati wa kubadilisha tahasusi.

Aliwataka wakuu wa shule za binafsi ambazo wanafunzi watathibitisha kujiunga nazo, kuthibitisha kuwatambua wanafunzi hao kupitia mfumo wa 'Selform'.

Ummy alibainisha idadi ya wanafunzi wenye sifa za kuchaguliwa kujiunga na kidato cha tano na vyuo vya elimu na mafunzo ya fundi imeongezeka kwa asilimia 14.07 kutoka wanafunzi 129,854 mwaka jana hadi 148,127 mwaka huu, akifafanua kwamba imetokana na ujenzi wa miundombinu.

## HABARI KITAIFA

# Rasimu Katiba Fungamano la Afrika Mashariki yaratibiwa

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, amesema wizara inaendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika maandalizi ya Rasimu ya Katiba ya Fungamano la Kisiasa la Afrika Mashariki kama hatua ya mpito kuelekea Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki.

Balozi Mulamula aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Alisema hadi kufikia Aprili mwaka huu, mchakato wa kukusanya maoni na kutoa elimu kwa umma ulikuwa umefanyika katika nchi za Burundi na Uganda.

Alisema kulingana na ratiba ya mchakato huo, timu ya wataalamu ya jumuiya inayokusanya maoni kuhusiana na rasimu ya katiba hiyo itatembelea Tanzania Agosti mwaka huu.

Alisema kuwa mwezi uliopita, wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika mkutano wa mawaziri wanaohusika na masuala ya kazi na ajira katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambapo nchi wanachama ziliweka msimamo wa pamoja kuhusu maboresho ya Katiba ya Shirika la Kazi Duniani.

Alisema marekebisho hayo yanalenga kuongeza wigo wa demokrasia katika uamuzi ndani ya shirika hilo.

"Msimamo huo wa nchi za SADC unatarajiwa kuwasilishwa katika vikao vya Umoja wa Afrika kwa majadiliano na kuweka msimamo wa pamoja wa nchi za Afrika kuhusu maboresho ya Katiba ya Shirika la Kazi Duniani," alisema.



Mafundi wa Kampuni ya Ujenzi ya Nyanza Road, wakipaka rangi kuweka alama ya kivuko cha waenda kwa miguu barabarani, eneo la Kitunda-Kivule, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# 'Mashehe, maimamu jiepusheni migogoro'

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma, Bashiru Husseni, amewapa angalizo viongozi wa dini hiyo kujiepusha na migogoro.

Waliopewa angalizo hilo ni mashehe, maimamu na walimu wa madrasa, wakitakiwa kujiweka kando na migogoro na kuzingatia kanuni na sheria za dini ya kislamu.

Husseni aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waumini na viongozi wa msikiti wa Mlimwa 'C' jijini hapa baada ya kumsimamisha Imamu Salehe Saidi na mzee Ahadi Kifimbo kwa tuhuma za kuhamasisha mgogoro.

Alisema hatua hiyo imechukuliwa baada ya kujiridhisha kuwa viongozi hao hukiuka sheria na kanuni za dini ya kislamu.

"Baraza kuu la waislamu Tanzania chini ya msimamizi wake mkuu, Shekhe Mkuu Mufti Abubakar Zuberi anatutaka viongozi wote kuanzia ngazi ya vitongoji mitaa vijiji kata wilaya mkoa hadi taifa kufanya kazi kwa kujitambua kwa kubadilika na acha mazoea," alisema.

**"Baraza kuu la waislamu Tanzania chini ya msimamizi wake mkuu, Shekhe Mkuu Mufti Abubakar Zuberi anatutaka viongozi wote kuanzia ngazi ya vitongoji mitaa vijiji kata wilaya mkoa hadi taifa kufanya kazi kwa kujitambua kwa kubadilika na acha mazoea," alisema.**

# Mwinyi asimulia kufukuzwa nyumba ya serikali kwa amri

**Na Christina Mwakangale**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amesimulia alivyofukuzwa kwenye nyumba ya serikali.

Katika kitabu cha 'Mzee Ruksa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi, anasema kuwa baada ya kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, anayeshughulikia Muungano, ilimlazimu kuhama mara moja kumpisha aliyechukua nafasi yake.

Anasema kuwa baada ya mabadiliko hayo ya Baraza la Mawaziri, makazi alimokuwa akiishi, ilibidi yachukuliwe na Jackson Makwetta.

Mwinyi anasema Makwetta hakuwa na subira kumpa muda wa kujiandaa kuhama, akimtaka ampishe mara moja.

"Niliporejea nchini (kutoka nje ya nchi) nilifikia Tandika. Baada ya muda nikateuliwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Baadaye tena nilibadilishwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, anayeshughulikia Muungano na ofisi ya wizara ilikuwa Zanzibar.

"Wakati ninaanza uhamisho huo, nilikuwa nimeanza ujenzi wa nyumba yangu ninamoishi.

"Oesterbay kwenye nyumba ya serikali nilimokuwa naishi kulikuwa na vifaa vyangu vya ujenzi... nondo, matofali...Makwetta akapangiwa nyumba;

"Hakuwa na subira kunipa muda wa kuhamisha vifaa vyangu vya ujenzi. Akaja nyumbani na kunitaka nimpishe...na kusema niende kwetu Zanzibar," anasema Mwinyi.

Anasema hakutaka ugomvi na kuamua kuondoka na kumwachia nyumba pamoja na vifaa vyake vya ujenzi kwenye nyumba hiyo.

"Nina uhakika hii ilimsumbua sana baadaye nilipokuja kuwa Rais, tena bila kinyongo nikaendelea kumpa uwaziri," Mwinyi anasimulia.

0000


bgtl

**BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **FNB BANK** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa wadaiwa wanaotajwa hapo chini, walipe madeni wanayodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) zilizodhamini mikopo yao kwa MNADA WA HADHARA.Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | HATIMA LIVINGSTONE SHAYO | Nyumba ya Makazi yenye **Hati ya** mauziano Na. 67782 Kiwanja Na.66 Kitalu "10" maeneo ya Tuangoma Manispaa ya **Temeke** kwa jina la **Hatima livingstone shayo.** | 26/06/2021 |
| 2. | FLORA KOKUNYWANISA RWEYEMAMU | Nyumba ya Makazi yenye **Hati ya** mauziano Nª. 135118 Kiwanja Na.40 Kitalu "R"maeneo ya Mapinga Dar es salaam kwa jina la **Flora Kokunywanisa Rweyemamu** | 19/06/2021 |
| 3. | DENIS KASHAIJA MUSHEMA | Nyumba ya Makazi yenye **Hati ya** mauziano Na. 53877 Kiwanja Na.159 Kitalu "1" maeneo ya Tuangoma Manispaa ya **Temeke** kwa jina la **Denis Kashaija Mushema.** | 26/06/2021 |
| 4. | LETICIA K RWEYEMAMU | Nyumba ya Makazi yenye **Hati ya** mauziano Na. 145883/1 - 145883/212 Kiwanja Na.44/2 iliyopo Mwongozo, Ghorofa na.623 Kitalu "6" Manispaa Kigamboni **kwa** jina la **Leticia K Rweyemamu.** | 26/06/2021 |
| 5. | DOTTO JOSEPH IBAMBASI. | Nyumba ya Makazi yenye **Hati ya** mauziano No. 92587 Kiwanja Na.15 Kitalu "CC"maeneo ya Tabata Manispaa ya **Ilala** kwa jina la **Dotto Joseph Ibambasi** | 30/06/2021 |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Building, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537**

**Au**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**First National Bank**
**1st Floor FNB House**
**Ohio Street**
**P. O. BOX 72290**
**DAR ES SALAAM**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Iwapo viroba vilikwisha, tumbaku inasubiri nini?

MWAKA 1987 Shirika la Afya Duniani (WHO) lilianzisha kampeni za kupinga matumizi ya tumbaku ambayo inaelezwa kuwa ilileta athari kwa binadamu na mazingira pia usumbufu uliokithiri, mathalani kilevi hicho kikitumika hata ndani ya ndege.

Ni miaka takribani 34 sasa tangu kuanza kwa hatua za kufikia dunia isiyotumia tumbaku. Lakini, licha ya jitihada hizo mikakati ya kukataza matumizi ya tumbaku nchini haijapewa msukumo mkali na kinachokera ni watu kuvuta sigara kwenye vituo vya mabasi, sokoni, barabarani na kwenye mikusanyiko bila kujali.

Kwa Tanzania hata serikali itakubaliana nasi kuwa matumizi ya tumbaku yapo zaidi kwenye sigara ambayo ni bidhaa inayotumiwa na kuuzwa kiholela kupindukia.

Karibu kila kona ya nchi hii biashara kubwa ni sigara ambazo huuzwa majumbani, wafanyabiashara wadogo wengi kila mahali kwani zina wateja wa kila aina hasa vijana na wazee.

Ndani ya vituo vya mabasi popote nchini sigara huvutwa muda wote na moshi unasambaa kwa kina mama na watoto wanaofanya biashara hiyo hasa maeneo ya mijini. Hao ndiyo wauza sigara, karanga, pipi, biskuti, vitafunuo na bidhaa ndogo ndogo zinazoliwa muda wote na abiria au wasafiri vituoni.

Ndiyo maana tunaona kuwa wakati umefika nchi imaanishe na ishiriki kikamilifu vita dhidi ya matumizi ya tumbaku kwa kuanza na kukataza kilimo na matumizi ya bidhaa zake ili kuwalinda wasiovuta kwani kutiba mgonjwa aliyeathiriwa na tumbaku ni mzigo kwa familia na taifa.

Serikali inasema asilimia 14 ya Watanzania hutumia tumbaku na kwamba Tanzania bila tumbaku inawezekana. Hata hivyo, haisemi inakomeshaje, lini na vipi matumizi ya tumbaku.

Magonjwa mengi yanahusishwa na kutumia tumbaku kama kuziba mishipa ya moyo na kusababisha shinikizo la juu la damu ambalo husababisha matibabu ya gharama kubwa kuizibua. Kwa mujibu wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, inaweza kugharimu Shilingi milioni 30.

Aidha, ni gharama kubwa kutibu magonjwa ya saratani tena ni hasara kwa taifa na pia ni hasara vijana kufariki wakiwa na uwezo mkubwa wa kufanyakazi.

Vifo hivyo ni sawa na maangamizo ya nguvu kazi ya nchi, mathalani vijana kupoteza maisha katika umri wa miaka 40 ni hasara kwa familia na taifa, ndiyo maana Tanzania inatakiwa kumaanisha kupiga vita matumizi ya tumbaku siyo kuendeleza blah blah.

Kama serikali iliweza kukataza matumizi ya pombe za viroba inashindikana nini kukomesha bidhaa za tumbaku kuanzia sigara, shisha, ugoro na kuberi? Ni dhahiri kuwa sigara ni kitanzi kwa taifa kwa vile inaua mamilioni ya wasiovuta wanaofikiwa na moshi na wale wanaoishi na wanaovuta.


Kwa mujibu wa WHO zaidi ya asilimia 70 ya magonjwa ya saratani ya mapafu na njia za hewa yana uhusiano na matumizi ya tumbaku ikiwamo sigara. Ina maana gani kuendelea kuruhusu biashara ya bidhaa ambayo inaangamiza Watanzania?

Tunaona kuwa licha ya maelezo kuwa tumbaku inaliingizia taifa fedha nyingi za kigeni na kuna uwekezaji wa kuzalisha sigara, wakati umefika kuchagua maisha badala ya fedha zinazotokana na mauzo ya biashara hiyo ambayo hutumika tena kutibu waathirika.

Tunaomba serikali isiishie kutoa takwimu ya idadi ya watumia tumbaku na magonjwa yanayotokana na kutumia bidhaa hiyo, badala yake ichukue hatua kuokoa maisha ya Watanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Sheria mpya usalama chachu utii wa sheria

Na Sabato Kasika

KATIKA awamu hii mambo ambayo yanahitaji kujadiliwa na kufanyiwa kazi ili kuleta tija kwa taifa ni suala la maboresho ya sheria ya usalama barabarani, ili iendane na hali halisi au zama za uendeshaji unaohitaji umakini unaoletwa na mabadiliko ya kiteknolojia.

Usalama barabarani unahusu sheria ambazo zinawalinda watumiaji barabara wakiwamo madereva, wanaotembea, vyombo vya moto, miundombinu - barabara, alama za utambulisho na madaraja.

Uwepo wa sheria hiyo ndiyo utakaofanikisha utekelezaji wa maagizo ya polisi ya utii wa sheria bila shuruti ili kupunguza ajali zinazoangamiza maisha, kuleta ulemavu na uharibifu wa rasilimali.

Ujio wa maboresho ya sheria za barabara utahakikisha kuwa kuna vipengele vinavyokataza au kutoa maelekezo ya kutumia simu barabarani, matumizi ya mikanda ya abiria, kofia ngumu kwa wanaotumia pikipiki, bajaji, ulinzi wa watoto kwenye pikipiki na kudhibiti kelele za muziki kwenye vyombo vya moto.

Sheria ni muhimu kwa sababu polisi kwa kushirikiana na wadau wengine mara kwa mara wanatoa elimu kwa madereva na watumia barabara ili eneo hilo lisiwe mahala pa kukatisha maisha ya watu, kuongeza vilema, kuharibu mali na chanzo cha hasara kwa taifa.

Hivi karibuni serikali ilitangaza kuwa jitihada za polisi na wadau kutoa mafunzo zimeanza kuzaa matunda, kwa kuwa hata kiwango cha makusanyo ya faini za makosa ya barabarani kinaelezwa kuwa kimepungua kutokana na wengi kutii sheria na kuelewa umuhimu wake.

Si kupungua kwa makusanyo tu, bali Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro, anasema, hata ajali za barabarani kuanzia Januari hadi Aprili mwaka huu zimepungua kwa asilimia 29.

Hizo zote ni juhudi za elimu kwa umma ambayo imesaidia kutii sheria za usalama barabarani bila shuruti. Polisi inasema kuanzia Julai 2019 hadi kufikia Julai mwaka jana, jumla ya Sh. bilioni 56 zilikusanywa, lakini sasa kiwango hicho kimepungua, ikiwa ni matokeo ya watu kutii na kuelewa umuhimu wa sheria.

Kwa hali hiyo, ni wazi elimu imekuwa na mchango mkubwa, hivyo ingependeza iwapo itaendelea kutolewa zaidi ili ikiwezekana, makusanyo ya fani yawe sifuri na ajali pia zizidhibitiwe.

Kupungua kwa makusanyo ya faini ya makosa ya barabarani na ajali, ni dalili za kutosha kwamba, elimu inazidi kuwaingia wahusika, hivyo si vibaya polisi kuendelea kuitoa na kubadilisha sura za barabara.

Makosa ya barabarani yamekuwa yakigharimu maisha ya watu kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo uzembe wa kutotii sheria ambazo kila dereva wa chombo cha moto na mtumiaji wa barabara anatakiwa kuzitii.

Wapo wanaotumia simu na kuweka foni masikioni, wanaotongoa (kuchati) wakiwa kwenye usukani, wanaowaendesha watoto kwenye pikipiki bila kuwa na mikanda wala kofia ngumu.

Si hayo tu kuna baadhi ya madereva wanaoendesha bajaji wakiwajaza abiria hadi kwenye kiti cha dereva mambo yanayoweka rehani maisha ya wateja wao.

Mafunzo yanawapa watumiaji wakiwamo abiria, wanaotembea na madereva maelekezo kulinda usalama wao na vitu vingine ndani ya barabara, hivyo zinapokuja taarifa za kupungua makusanyo ya fedha za faini kwa kushuka kwa kiwango cha ajali, ni wazi polisi wanafanya kazi kwa tija.

Polisi kukusanya fedha kidogo kutokana na faini, iwe ni fursa kwao kuendelea kujikita zaidi kwenye utoaji wa elimu kwa watumiaji wa barabara, kwa kuwa imeanza kuleta matokeo chanya kwani fedha hazina maana iwapo watu watapoteza maisha, ongezeko la walemavu, barabara kuharibiwa na taifa kupata hasara.

Idadi hiyo ya waliopata elimu ya usalama barabarani na kutii sheria ikiendelea kuongezeka, huenda hakutakuwa na faini tena na ajali pia zitapungua na usalama na ulinzi wa Watanzania utakuwa kipaumbele.

**HABARI KITAIFA**

# Mbaroni tuhuma za kumiliki sare za JWTZ

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MKULIMA wa Kata ya Kihonda Manispaa ya Morogoro, Amiri George (22) anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani hapa kwa tuhuma za kukutwa akimiliki sare za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) nyumbani kwake.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Muslim, alisema kuwa tukio hilo lilitokea Mei 25, majira ya saa 9 usiku katika eneo la Kihonda Bima Manispaa ya Morogoro, kwamba askari waliokuwa doria walimkamata mtuhumiwa huyo akiwa na sare za JWTZ.

Kamanda Muslim alisema mtuhumiwa huyo alikutwa na kofia tatu na fulana moja za jeshi ambazo alikuwa amezihifadhi ndani kwake kwenye chumba anachoishi jambo ambalo ni kosa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Alisema kwa sasa mtuhumiwa huyo anahojiwa na polisi na kwamba atafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi mkoani Morogoro linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kupatikana na silaha mbili za aina tofauti bila kibali.

Kamanda Muslim aliwataja wanaoshikiliwa kuwa ni Greyson Basil (41) Mkazi wa Kijiji cha Mpanga na Edson Aluti (46) pamoja na Juma Joseph wote wakiwa ni wakazi wa kijiji cha Matangini Mlimba.

Kamanda Muslim alisema watuhumiwa wote kwa pamoja walikamatwa na askari waliokuwa doria Machi 23, mwaka huu majira ya saa 12 asubuhi katika Kijiji cha Mpanga, Tarafa ya Mlimba wilayani Kilombero.

Alisema mtuhumiwa wa kwanza Basil alikamatwa akiwa na silaha moja aina ya Mark IV ikiwa imefukiwa ardhini.

Kamanda Muslimu alisema msako huo uliendelea na kufanikiwa kuwakamata Aluta na Joseph wakiwa na silaha aina ya gobole, maganda nane ya risasi za bunduki aina ya shortgun.

Pia walikamata gorori 39 kwenye maeneo ya kitalu cha uwindaji North Safari kilichopo Kata ya Utengule Tarafa ya Mlimba.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima, akigawa maziwa kwa wanafunzi wakati wa maadhimisho ya uzinduzi wa Wiki ya Maziwa, katika viwanja vya Tangamano, jijini Tanga jana. PICHA: HAMIDA KAMCHALLA

# ‘Kero za watumishi pembezoni zitatuliwe’

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dk. Laurean Ndumbaro, amewataka viongozi katika taasisi za umma kutumia maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka huu kutembelea maeneo ya pembezoni ili kusikiliza na kutatua kero zinazowakabili.

Dk. Ndumbaro alitoa agizo hilo juzi katika Tarafa ya Karema mkoani Katavi akiwa ameambatana na Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria Prof. Sifuni Mchome, na Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, ambao kwa pamoja walihimiza uwajibikaji na ufanisi kiutendaji katika taasisi zinazosimamia utoaji wa haki kwa wananchi.

Aliwataka viongozi katika taasisi za umma kuhakikisha wanajenga utamaduni wa watumishi kufanya kazi kwa bidii na kuongeza kuwa utamaduni huo utajengwa kwa kutambua na kuwapongeza wanaofanya kazi kwa juhudi na maarifa na kwa wanaolegalega warekebishwe ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Alifafanua kuwa, watumishi wanaochapa kazi wakipongezwa kwa kuandikiwa barua au kupewa cheti kutokana na mchango wao, ndiyo njia pekee itakayowawezesha waajiri kujenga utamaduni wa watumishi kufanya kazi kwa bidii na weledi.

Akizungumzia kuhusu mtazamo hasi wa baadhi ya watumishi wa Tarafa ya Karema kuamini kuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu, Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. Jingu, aliwataka kubadili fikra zao kwa kuwa serikali imewaajiri kwa lengo la kuwahudumia wananchi wa eneo hilo na si kuwapa adhabu kama baadhi yao wanavyodhani.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUITWA KUANZA USAJILI WA MAFUNZO YA STADI ZA KAZI KATIKA FANI MBALIMBALI KWA NJIA YA UANAGENZI**

Itakumbukwa kuwa tarehe 15 Aprili, 2021, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu ilitangaza fursa za mafunzo ambayo yatatolewa katika taasisi za mafunzo zilizotangazwa kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara. Ofisi ya Waziri Mkuu inapenda kuuarifu umma kuwa, vijana 14,440 wamechaguliwa kujiunga na mafunzo katika vyuo 72 nchini. Majina ya vijana waliochaguliwa yamebandikwa kwenye mbao za matangazo za vyuo husika na katika tovuti za: www.pmo.go.tz na www.kazi.go.tz. Vijana waliochaguliwa wanatakiwa kuripoti kwenye vyuo hivyo kwa ajili ya kuthibitisha ushiriki wao na kujisajili kuanzia tarehe 2 Juni, 2021. Mikoa na vyuo husika ni kama ifuatavyo:-

| MKOA | JINA LA CHUO |
|---|---|
| ARUSHA | 1. CHUO CHA TAIFA CHA UTALII – ARUSHA KAMPASI |
| | 2. ARUSHA VTC - VETA |
| | 3. VETA NJIRO |
| | 4. HELP TO SELF HELP ORGANIZATION |
| DAR ES SALAAM | 5. CHUO CHA VETA – CHANG’OMBE |
| | 6. VETA KIPAWA |
| | 7. CHUO CHA TAIFA CHA UTALII – BUSTANI KAMPASI DSM |
| DODOMA | 8. VETA DODOMA |
| GEITA | 9. CHATO DVTSC |
| IRINGA | 10. VETA IRINGA RVTSC |
| | 11. ILULA FDC |
| | 12. RDO MDABULO VTC (MAFINGA) |
| | 13. RDO MDABULO VTC (KILOLO) |
| | 14. MAFINGA LUTHERAN VTC |
| | 15. INCOMET VTC MAFINGA |
| KAGERA | 16. VETA KAGERA |
| | 17. GERA VTC, MISENYI |
| KATAVI | 18. VETA MPANDA RVTSC |
| KIGOMA | 19. VETA KIGOMA |
| | 20. KASULU FDC |
| | 21. NYAMIDAHO VTC, KASULU |
| | 22. KIBONDO FDC |
| KILIMANJARO | 23. VETA – MOSHI RVTSC |
| | 24. KILIMANJARO INDUSTRIAL DEVELOPMENT TRUST-MOSHI |
| | 25. MOSHI INSTITUTE OF TECHNOLOGY - MOSHI |
| LINDI | 26. CHUO CHA VETA -LINDI |
| MANYARA | 27. VETA – MANYARA RVTSC |
| MARA | 28. LAKE VICTORIA DISABILITY VOCATIONAL CENTRE |
| | 29. KISANGWA FDC |
| | 30. VETA MARA |
| MBEYA | 31. VETA BUSOKELO DVTC, MBEYA |
| | 32. KYELA POLYTECHNIC COLLEGE |
| | 33. VETA MBEYA RVTSC |
| | 34. MAGEREZA RUANDA VTC MBEYA |
| | 35. MBEYA UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY (MUST) |
| MOROGORO | 36. IFAKARA FDC |
| | 37. VETA MIKUMI VTC |
| | 38. UMOJA WA MAFUNDI KABAMBE VTC |
| | 39. VETA KIHONDA RVTSC |
| | 40. VETA DAKAWA VTC |
| MTWARA | 41. CHUO CHA VETA - MTWARA |
| | 42. MTAWANYA FDC |
| MWANZA | 43. VETA- MWANZA RVTSC |
| | 44. SENGEREMA FDC |
| | 45. MWANZA ISLAMIC CENTER, ILEMELA |
| | 46. NYAKATO VTC |
| NJOMBE | 47. NJOMBE FDC |
| | 48. ULEMBWE FDC |
| | 49. CHUO CHA VETA - MAKETE |
| PWANI | 50. VETA – PWANI RVTSC |
| | 51. IKWIRIRI FDC |
| | 52. VIKINDU CATHOLIC POLYTECHNIC COLLEGE |
| | 53. KISARAWE FDC |
| RUKWA | 54. KATANDALA VTC |
| | 55. LAELA AGRICULTURAL VTC |
| | 56. MVIMWA VTC NAMANYERE |
| | 57. TAASISI YA MAFUNZO YA AFYA YA ST. BAKHITA |
| | 58. CHALLA FDC NAMANYERE |
| RUVUMA | 59. CHUO CHA VETA - SONGEA |
| | 60. VETA NAMTUMBO |
| | 61. CHUO CHA UFUNDI STADI KIUMA, TUNDURU |
| SHINYANGA | 62. VETA SHINYANGA |
| | 63. MWANVA FDC KAHAMA |
| SIMIYU | 64. CHUO CHA UFUNDI BINZA (BINZA VCT) |
| SINGIDA | 65. SINGIDA FDC |
| | 66. SABASABA CHUO CHA ULEMAVU |
| | 67. VETA SINGIDA |
| | 68. ILEJE DVTC - SONGWE |
| | 69. DIT MYUNGA |
| TABORA | 70. VETA TABORA |
| | 71. VETA ULYANKULU |
| TANGA | 72. VETA – TANGA RVTSC |

**IMETOLEWA NA:**
**KATIBU MKUU**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Udhalilishaji wa mtandaoni tishio

**Na Mary Geofrey**

KUTOKANA na kuongezeka kwa watumiaji wa mtandao nchini, serikali imeombwa kuweka sheria ya kudhibiti matukio ya ukatili wa kijinsia mitandaoni.

Kwa mujibu wa takwimu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), hadi mwaka 2017, watumiaji wa mitandao waliongezeka kwa asilimia 16 na kufikia milioni 23 na asilimia 82 kati yao walitumia kwa njia ya simu.

Ombi hilo limetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na masuala ya wanawake (UN-Women), Phumzile Mlambo-Ngucka, mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, alipokutana na asasi za kiraia zinazopigania haki za wanawake.

"Tanzania kuna maeneo mawili ambayo yenye ukatili wa kijinsia, kupitia mitandao ya kijamii na siasa. Kuna haja sasa ya serikali kuona namna ya kuweka sheria ya kudhibiti vitendo hivi," alisema Dk. Mlambo Ngucka.

Alisema wamekuwa wakishuhudia video za utupu za wanawake na watoto wa kike zikisambazwa katika mitandao hiyo kwa makusudi.

Alifafanua kuwa, udhalilishaji huo una madhara kisaikolojia na kusababisha kuathirika kisaikolojia kunakowafanya watu kujiua au kupoteza mwelekeo katika maisha.

Dk. Mlambo Ngucka, ambaye yupo nchini kwa lengo la kusukuma ajenda ya usawa na zaidi uongozi wa wanawake kuelekea mkutano wa Generation Equality unaotarajiwa kufanyika Juni 20 hadi Julai 2, nchini Ufaransa, alisema wanawake wa Tanzania wanapaswa kuongoza nyanja zote si tu za kisiasa hata kwenye taasisi binafsi.

Alisema uwakilishi wa wanawake katika uongozi bado hautoshi kote duniani na sasa ni wakati wa kukamilisha malengo ya mkutano wa Beijing kuhusu haki za wanawake katika kila nyanja.

Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Africa (WILDAF), Anna Kulaya, alisema woga na kutojiamini miongoni mwa wanawake nchini ni changamoto kubwa. Kulaya alisema ni wakati sasa wa asasi za kitaifa na serikali kutoa elimu na kuwajengea uwezo na badala ya kusubiri hadi kipindi cha uchaguzi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania ( TGNP), Lilian Lihundi, alisema ukosefu wa fedha ni changamoto kubwa kwa asasi za kiraia kushindwa kuwafikia wanawake wengi hususani waliopo vijijini.



Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim Tanzania, Stanley Kafu (wa pili kushoto), akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ndatwa Ludigija (katikati), vifaa vya usafi vilivyotolewa na benki hiyo, ili kuimarisha hali ya usafi katika Jiji la Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambayo kilele chake kinatarajiwa kuwa Juni 5, mwaka huu. Wengine ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilala, Charangwa Makwiro (watatu kushoto) na pamoja na wafanyakazi wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tigo kupanda miti 28,000 Mlima K'njaro

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi Tigo, inatarajia kupanda miti 28,000 mwaka huu, katika eneo la kuzunguka Mlima Kilimanjaro katika kuadhimisha Siku ya Mazingira.

Mkurugenzi Mkuu wa Tigo, Simon Karikari, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mpango huo, alisema kampeni hiyo iliyopewa jina la Tigo Green For Kili, iliyozinduliwa Februari 27, mwaka huu.

Alisema amechangia miti 100 ili kuwashawishi wakurugenzi wenzake akiwamo wa Benki ya Standard Chartered, Sanjay Rughani kuchangia kampeni hiyo.

Alisema kampeni hiyo inaenda sambamba na kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani ambayo hufanyika Juni 5, kila mwaka.

"Kwa niaba ya Tigo Tanzania, ninachukua fursa hii kuwashukuru wote waliojitokeza kutuunga mkono kuchangia kupanda miti ambayo itakuwa sehemu mojawapo ya kulinda na kuendeleza mazingira kwenye eneo la Mlima Kilimanjaro," alisema Karikari.

Alisema kauli mbiu ya mwaka huu inasema, 'Kurejesha Mfumo wa Ikolojia', hivyo aliwataka wadau kushiriki hafla ya kupanda miti viwanja vya Half London, Moshi mkoani Kilimanjaro.

"Kwa niaba ya Tigo Tanzania, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru wadau wote walioitikia wito huu na kuchangia ili kuifanya Kilimanjaro iwe ya Kijani tena," alisema Karikari.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Henry Kinabo, alisema wanaamini miti hiyo ikitunzwa vizuri italeta manufaa makubwa ikiwamo kutunza mazingira yanayozunguka Mlima Kilimanjaro.

"Tunafurahia kushirikiana na wadau mbalimbali katika kufanikisha kampeni hii ambayo itakua endelevu na miti ikitunzwa vizuri ni faida kwetu kwa baadaye.

"Hii ndio sababu kama Tigo, tuna kauli mbiu isemayo 'One Step, One Tree' kwa ajili ya kuunganisha nguvu ili kuhifadhi Mlima Kilimanjaro ambao utasaidia kuleta maendeleo endelevu ya mkoa na taifa kwa ujumla.

# Jiji Dar lapewa vifaa vya usafi

**Na Mwandishi Wetu**

JIJI la Dar es Salaam limekabidhiwa vifaa vya usafi ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambayo kilele chake kinatarajiwa kuwa Ijumaa.

Vifaa hivyo vimekabidhiwa na Benki ya Exim kwa halmashauri hiyo.

Ikiwa ni hatua ya mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo wa kutunza mazingira unaofahamika kama Exim Go Green Initiative.

Akipokea msaada huo jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ndatwa Ludigija, pamoja na kuishukuru benki hiyo kwa msaada huo, alizialika taasisi mbalimbali kushiriki kwenye utunzaji wa maeneo ya asili ikiwamo fukwe za bahari, kupanda miti na maua kwenye maeneo ya wazi na hifadhi za barabara pamoja kuhifadhi bustani zilizopo maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

"Jitihada kama hizi zinazoonyeshwa na Benki ya Exim sambamba na shughuli nyingine nyingi zitaendelea wiki nzima kuanzia Juni mosi hadi Juni 5 ambayo ndio siku ya kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mazingira," alibainisha Ng'wilabuzu, huku akiwahimiza makandarasi wanaotoa huduma ya uzoaji taka katika jiji hilo kuhakikisha wanakuwa na vifaa vya kutosha na kutoa huduma inayokidhi mahitaji ya wananchi kwa wakati.

Alisema maadhimisho hayo yataambatana na shughuli mbalimbali inayolenga kuongeza hamasa za utunzaji wa mazingira ikiwamo mikutano ya kitaaluma juu ya masuala ya mazingira, matamasha ya maonyesho, kampeni za usafi wa mazingira, shughuli ambazo zitaendelea kwa wiki nzima kuanzia Juni mosi.

Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano Benki ya Exim, Stanley Kafu, alisema msaada huo unahusisha vifaa mbalimbali vya kufanyia usafi ikiwamo matoroli ya kubebea takataka, vyombo vya kuhifadhi takataka, mafagio, reki pamoja na makoleo.

"Siku ya Mazingira Duniani ni siku ambayo inahitaji jitihada za pamoja ili kuhakikisha suala zima la usafi na mwonekano wa mazingira linapatiwa ufumbuzi. Hiyo ndio sababu Benki ya Exim tunaamini sana umuhimu wa kusaidia mipango ya mazingira ambayo ina faida za moja kwa moja kwa jamii," alisema Kafu.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI



BALOZI LIBERATA RUTAGERUKA MULAMULA (MB),
*WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI*



MHE.BALOZI MBAROUK NASSER MBAROUK (MB)
*NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI*



BALOZI JOSEPH EDWARD SOKOINE
*KATIBU MKUU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI*



BALOZI FATMA MOHAMMED RAJAB
*NAIBU KATIBU MKUUU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI*

# HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI LIBERATA RUTAGERUKA MULAMULA (MB), WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

# HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI LIBERATA RUTAGERUKA MULAMULA (MB), WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**1.0 UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 20-20-21 na pia lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 20-21-22. Aidha, naomba Hotuba yangu yote kama ilivyo kwenye Kitabu cha Bajeti iingizwe kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge (Hansard).

2. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu siku ya leo. Kwa kuwa Hotuba hii ya Bajeti ni ya kwanza nikiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuongoza Wizara hii. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa nitafanya kazi kwa uwezo wangu wote na kwa kudra za Mwenyezi Mungu nitatekeleza majukumu yangu ipasavyo katika kuleta maendeleo ya Taifa letu.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kwamba, tarehe 17 Machi, 2021 Taifa lilipata msiba mzito wa kuondokewa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Taifa letu limepoteza viongozi wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Balozi Mhandisi John William Hebert Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Naomba kutumia nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu waliotangulia kuwasilisha Hotuba zao kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais, familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa misiba hii mizito. Wizara yangu inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa viongozi hawa katika kukuza diplomasia yetu.

4. ***Mheshimiwa Spika***, natumia nafasi hii pia kutoa shukrani za dhati kwa nchi marafiki na jumuiya ya kimataifa kwa kuonesha mshikamano, kutufariji na kushiriki nasi katika kipindi cha majonzi makubwa kwa Taifa letu.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee naomba kutoa shukrani kwa Umoja wa Mataifa kwa uamuzi wake wa kuitisha kikao rasmi cha Baraza Kuu la Umoja huo kwa ajili ya kumuenzi na kumkumbuka Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia kikao hicho, Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa zilielezea mafanikio makubwa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaliyopatikana chini ya Uongozi wa Hayati Dkt. Magufuli katika kuboresha huduma za jamii kama vile elimu, maji, afya, nishati na miundombinu ya usafirishaji. Tunawashukuru sana.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, naomba kutoa pole kwako na Bunge lako Tukufu kufuatia vifo vya Waheshimiwa Khatibu Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde; Mhandisi Atashasta Justus Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe Mkoa wa Kigoma; na Martha Jachi Umbulla aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu mahala pema peponi. Amina.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa na kwa moyo mkunjufu napenda kutumia nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), kwa kuaminiwa kuendelea kushika nafasi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Othman Masoud Othman Sharif kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** tuna imani kuwa uongozi mpya utaendelea kudumisha tunu za Taifa na kuimarisha diplomasia ya nchi yetu.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imeweka historia ya kujivunia na kuigwa duniani kwa namna ilivyopata uongozi wa juu wa Serikali kwa kuzingatia misingi ya Katiba kufuatia vifo vya Viongozi Wakuu waliokuwa madarakani. Hatua hii ni kielelezo cha ukomavu, uimara wa demokrasia na kuzingatiwa misingi ya utawala wa sheria.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake aliyowasilisha hapa Bungeni ambayo imetoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa kazi za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 20-21-22. Nawapongeza pia

Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hotuba zao katika Bunge hili la Bajeti.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako madhubuti katika uendeshaji wa

*Inaendelea Uk 11*

Inatoka Uk 10

shughuli za Bunge. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Naibu Spika; Wenyeviti wa Bunge; na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi nzuri wanazozifanya kukusaidia kusimamia na kuendesha shughuli za Bunge.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Uenyekiti wa Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb), pamoja na Makamu wake Mhe. Vincent Paul Mbogo (Mb), kwa kazi nzuri na ya kizalendo ya kuishauri Serikali hususan Wizara yangu. Naomba nikiri kuwa miongozo na ushauri wao katika masuala mbalimbali umekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kuwapongeza Waheshimiwa Eliadory Felix Kavejuru na Dkt. Florence George Samizi kwa kuchaguliwa hivi karibuni kuwa Wabunge wa Majimbo ya Buhigwe na Muhambwe, mtawalia. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa kuaminiwa kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili Tukufu. Vilevile, nitumie nafasi hii kuwapongeza viongozi wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa mbalimbali Serikalini. Kuteuliwa kwao ni kielelezo cha kuaminiwa na Mheshimiwa Rais katika kuwaletea maendeleo wananchi.

**2.0 MISINGI YA SERA YA TANZANIA KATIKA UHUSIANO WA KIMATAIFA**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** historia ya nchi yetu imesheheni misingi imara inayoiwezesha kuendelea kuwa miongoni mwa nchi zilizo na ushawishi mkubwa kimataifa tangu Uhuru. Misingi ya nchi yetu kuheshimika kimataifa iliwekwa na Waasisi wa Taifa letu kwa kupinga na kulaani ubabe, uonevu na ukandamizaji popote pale ulipotokea duniani bila hofu. Hivyo, katika kusimamia misingi hiyo, tumeendelea kulinda uhuru wetu; kujiamulia mambo yetu wenyewe bila kuingiliwa; kulinda mipaka ya nchi yetu; kutetea haki; kuimarisha ujirani mwema; na kutekeleza Sera ya Kutofungamana na Upande Wowote kama dira na msimamo wetu kwenye uhusiano na nchi nyingine katika jumuiya ya kimataifa.

**3.0 TATHMINI YA HALI YA UCHUMI, SIASA, ULINZI NA USALAMA DUNIANI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

16. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa taarifa fupi kuhusu hali ya uchumi, siasa, ulinzi na usalama duniani kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama ifuatavyo:

17. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia ya mwezi Januari 20-21, ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 20-20 ulipungua kwa asilimia 4.3 kutokana na janga la UVIKO-19 ambao uliathiri sekta nyingi za uchumi hususan uwekezaji, uzalishaji, upatikanaji wa huduma na biashara ya kimataifa. Kasi ya kupungua kwa ukuaji wa uchumi ilikuwa ndogo kwa asilimia 0.9 ikilinganishwa na makadirio ya awali ya asilimia 5.2. Aidha, kwa mwaka 20-21 uchumi wa dunia unakadiriwa kukua kwa asilimia 4 kutokana na kuanza kurejea kwa shughuli za kiuchumi katika nchi mbalimbali.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya siasa, ulinzi na usalama imeendelea kuimarika katika maeneo mengi barani Afrika. Katika kipindi cha mwezi Julai, 20-20 hadi Aprili, 20-21 nchi za Benin, Burkina Faso, Côte d'Ivoire, Chad, Ghana, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Niger, Shelisheli, Guinea, Uganda na Jamhuri ya Kongo zilifanya uchaguzi. Tunawapongeza Waheshimiwa Marais wa nchi hizo kwa kuchaguliwa na tunaahidi kuendelea kushirikiana na Serikali zao kwa lengo la kudumisha uhusiano baina ya nchi zetu.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** taarifa ya kina inapatikana kwenye **Aya ya 20** hadi **35** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**4.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

20. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha 20-20-21, Wizara yangu iliendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Muundo wa Wizara Toleo la tarehe 7 Julai, 20-18. Majukumu hayo yameainishwa kwenye **Aya ya 36** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa majukumu ya Wizara uliongozwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 20-15; Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 20-01; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 20-25; Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na miongozo mingine kama ilivyoainishwa kwenye **Aya ya 37** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

22. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, Wizara ilipanga kukusanya **shilingi bilioni mbili, milioni mia tano hamsini, laki nane na sabini na tisa elfu**. Kati ya kiasi hicho **shilingi milioni arobaini na saba, laki moja na sabini elfu** ni makusanyo ya Makao Makuu ya Wizara, na **shilingi bilioni mbili; na milioni mia tano na tatu na laki saba na elfu tisa** ni makusanyo kutoka Balozi za Tanzania. Vyanzo vya mapato hayo ni uhakiki wa nyaraka, pango la majengo ya Serikali nje ya nchi na mauzo ya nyaraka za zabuni.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 20-21, Wizara ilikusanya jumla ya **shilingi milioni mia saba hamsini na sita, laki moja themanini na mbili elfu na themanini na mbili** sawa na asilimia **ishirini na tisa nukta sita** ya lengo lililopangwa kwa Mwaka wa Fedha 20-20-21. Kupungua kwa mapato hayo kumetokana na kukosekana kwa wapangaji katika baadhi ya majengo ya Serikali kwenye Balozi za Tanzania kutokana na athari za uwepo wa janga la UVIKO-19 ambayo imesababisha kukosa wapangaji kutokana na kutokuwepo kwa biashara.

**Fedha Zilizoidhinishwa**

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 20-20-21, Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha **shilingi bilioni mia moja na tisini na tisa,**

Inaendelea Uk 12

Inatoka Uk 12

**milioni mia saba hamsini, laki sita themanini na nne elfu.** Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni mia moja sabini na tisa, milioni mia saba hamsini, laki sita themanini na nne elfu** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida; na **shilingi bilioni ishirini** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, **shilingi bilioni mia moja sitini na saba, milioni mia saba na kumi na saba, laki saba ishirini na tatu elfu** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na **shilingi bilioni kumi na mbili na milioni thelathini na mbili, laki tisa na sitini na moja elfu** ni kwa ajili ya Mishahara.

**Fedha Zilizopokelewa na Kutumika**

25. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 20-21 Wizara ilipokea kutoka Hazina kiasi cha **shilingi bilioni mia moja ishirini na saba, milioni mia sita arobaini na nane, laki tano arobaini na tisa elfu, mia tano kumi na tano**. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia **sitini na tatu nukta tisa** ya fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 20-20-21. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni mia moja kumi na nane, milioni mia nane tisini na tatu, laki tatu kumi na tisa elfu, mia tisa arobaini na saba** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo sawa na asilimia **sabini nukta tisa** na **shilingi bilioni nane, milioni mia saba hamsini na tano, laki mbili tisini na tisa elfu, mia tano sitini na nane** ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia **sabini na mbili nukta nane**.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika fedha zilizotolewa, Wizara ilitumia kiasi cha **shilingi bilioni mia moja na sita, milioni mia sita na moja, laki mbili hamsini elfu na mia tatu** sawa na asilimia **themanini na tatu nukta tano** ya fedha zilizopokelewa. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni tisini na saba, milioni mia nane arobaini na sita, ishirini elfu na mia saba thelathini na mbili** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **shilingi bilioni nane, milioni mia saba hamsini na tano, laki mbili ishirini na tisa elfu, mia tano sitini na nane** ni mishahara.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba sasa nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 20-20-21 kama ifuatavyo:

**4.1 Kusimamia na Kuratibu Masuala ya Uhusiano Baina ya Tanzania na Nchi Nyingine**

28. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Mei 20-21, Wizara iliratibu na kufanikisha Ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Kenya kufuatia mwaliko wa Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya. Ziara hiyo ya kwanza ya Kitaifa tangu kuapishwa kwa Mheshimiwa Rais ililenga kuimarisha uhusiano wa kidugu na ujirani mwema kati ya nchi hizi mbili. Wakati wa ziara hiyo, Mheshimiwa Rais alihutubia Kikao Maalum cha Pamoja cha Bunge la Taifa na Bunge la Seneti la Kenya.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Aprili 20-21, Wizara iliratibu ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Uganda. Wakati wa ziara hiyo, Mheshimiwa Rais na mwenyeji wake Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda walishuhudia uwekaji saini mikataba mitatu ya utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani - Tanga, Tanzania. Mikataba iliyosainiwa imeainishwa kwenye **Aya ya 50** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Januari 20-21, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Filipe Jacinto Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji hapa nchini kwa mwaliko wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika ziara hiyo, viongozi hao walikubaliana kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizi mbili na kukuza kiwango cha biashara na uwekezaji pamoja na kuimarisha ujirani mwema.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Januari 20-21, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Sahle-Work Zewde, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia iliyofanyika nchini. Tanzania na Ethiopia zilikubaliana kuongeza kiwango cha biashara na uwekezaji; kubadilishana utaalam na uzoefu katika uendeshaji wa viwanda vya kuongeza thamani ya ngozi za mifugo na Tanzania kuisaidia Ethiopia kufundisha lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Addis Ababa na Chuo cha Diplomasia cha Ethiopia.

32. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Oktoba 20-20, Wizara iliratibu ziara rasmi ya Mheshimiwa Dkt. Lazarus McCarthy Chakwera, Rais wa Jamhuri ya Malawi iliyofanyika nchini. Katika ziara hiyo, pamoja na mambo mengine, Tanzania na Malawi zilikubaliana kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani (OSBP) cha Songwe/ Kasumulu; ujenzi wa barabara ya Mpemba - Isongole – Mbozi -Chitipa - Mbilima; na Mamlaka ya Bandari Tanzania kufungua ofisi nchini Malawi. Nchi hizi pia zilikubaliana kushirikiana katika utekelezaji wa miradi ya pamoja ya kufua umeme na umwagiliaji katika Bonde la Mto Songwe.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Septemba 20-20, Wizara iliratibu ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda iliyofanyika nchini. Katika ziara hiyo, Tanzania na Uganda zilisaini Hati ya Makubaliano Kuanza Ujenzi wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani - Tanga, Tanzania. Maelezo ya kina ni kama inavyoonekana kwenye **Aya ya 46 hadi 61** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

34. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Januari 20-21, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mhe. Wang Yi, Mjumbe wa Baraza la Taifa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Watu wa China iliyofanyika hapa nchini. Pamoja na masuala mengine Serikali ya nchi hiyo ilitoa msaada wa shilingi **milioni mia tatu hamsini** kwa ajili ya kununua vifaa vya karakana ya fani ya uvuvi katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi VETA, Chato na Mwezi Mei, 20-21 imetoa msaada wa Shilingi

Inaendelea Uk 13

Inatoka Uk 13

**bilioni thelathini na tano nukta tatu saba** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo hapa nchini.

35. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Novemba 20-20, Wizara ilifanikisha kusainiwa kwa Mkataba kati ya Tanzania na China utakaowezesha Tanzania kuuza maharage aina ya soya katika soko la China. Kupitia Mkataba huo Tanzania inakuwa nchi ya 12 kuruhusiwa kuuza maharage hayo ambayo yana soko kubwa nchini humo. Kampuni 49 za Tanzania zimepata vibali vya kuuza maharage hayo katika soko hilo. Hadi kufikia mwezi Mei 20-21, zaidi ya tani **mia moja na ishirini** za soya zimekwishauzwa chini ya mpango huu**.**

36. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kufanikisha upatikanaji wa kampuni ya PT Indesso ya nchini Indonesia iliyojenga kiwanda cha kutengeneza mafuta yatokanayo na majani ya mimea katika eneo la Mgelema, Pemba kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Biashara la Zanzibar kwa gharama ya Dola za Marekani **milioni moja nukta nne**. Kiwanda hicho kilizinduliwa mwezi Septemba 20-20 na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Maelezo ya kina ni kama inavyoonekana kwenye **Aya ya 62 hadi 72** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi, Wizara imefanikisha Tanzania kuruhusiwa kuanza kuingiza nyama na bidhaa za nyama katika masoko ya nchi za Oman, Kuwait na Qatar. Vilevile, bidhaa hizo zitaanza kuuzwa nchini Saudi Arabia baada ya kukamilika kwa taratibu za kupata ithibati kutoka kwenye mamlaka za nchi hiyo. Aidha, mwezi Januari 20-21, Wizara ilifanikisha upatikanaji wa vibali kwa kampuni nane za Tanzania kuuza minofu ya samaki aina ya sangara katika nchi ya Saudi Arabia.

38. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Januari 20-21, Wizara ilifanikisha uwekaji saini Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mamlaka ya Uwekezaji ya Oman kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mangapwani, Zanzibar. Mradi huo utajumuisha ujenzi wa eneo la kuhudumia mizigo; gati la meli za uvuvi; gati la meli za mafuta na gesi; chelezo kwa ajili ya matengezo ya meli; na mji wa kisasa katika eneo la Mangapwani. Mradi utakapokamilika utachochea ukuaji wa biashara na usafirishaji Zanzibar.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Agosti 20-20, Wizara ilifanikisha kusainiwa kwa Mkataba wa mkopo wa Dola za Marekani **milioni kumi na tano nukta tatu** kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait kwa ajili ya mradi wa kilimo cha umwagiliaji kwenye eneo la ukubwa wa hekta **elfu tatu** katika Bonde la Mto Luiche mkoani Kigoma. Mradi huo utaongeza uzalishaji wa mazao ya mpunga, mahindi na mbogamboga na hivyo kuinua kipato cha wakulima wa eneo hilo. Maelezo ya kina ni kama inavyoonekana kwenye **Aya ya 73 hadi 81** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Februari 20-21, Wizara iliratibu uwekaji saini Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kampuni ya Tangen & Intertorco Group ya nchini Hispania kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri, Unguja; Bandari ya Mkoani, Pemba; na mradi wa kufua umeme kwa kutumia gesi. Hafla ya uwekaji saini makubaliano hayo ilishuhudiwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Desemba 20-20, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 111 wa Baraza la Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya OACPS uliofanyika kwa njia ya mtandao chini ya uenyekiti wa Tanzania. Kupitia Mkutano huo, Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi 10 za Jumuiya hiyo zitakazonufaika na utekelezaji wa mradi wa kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao ya samaki ujulikanao kama FISH4ACP unaogharimu shilingi **bilioni mia moja na kumi**. Katika mradi huo Tanzania imetengewa kiasi cha **shilingi bilioni 8** kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao ya samaki aina ya migebuka na dagaa kutoka mkoa wa Kigoma.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Oktoba 20-20, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa Mkataba kati ya Tanzania na Uswisi wa msaada wa shilingi **bilioni thelathini na tisa nukta moja tano** kugharamia utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini nchini na Mkataba wa shilingi **bilioni nne nukta tisa tano** ikiwa ni msaada wa kuchangia Mfuko wa Pamoja wa Afya. Pia, Wizara iliratibu kusainiwa kwa Mkataba kati ya Tanzania na Uswisi wa shilingi bilioni **kumi na tano nukta nane** ikiwa ni msaada kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Kutokomeza Malaria Awamu ya Kwanza; na Mkataba wa shilingi **bilioni ishirini na nne nukta saba sita** ikiwa ni msaada kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuimarisha Mfumo wa Kutoa Huduma za Afya Awamu ya Tatu. Misaada hiyo imeendelea kuchangia jitihada za Serikali katika kupunguza umaskini na kuboresha huduma za afya nchini.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina ni kama inavyoonekana katika **Aya ya 82 hadi 97** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

### 4.2 Kuratibu Masuala ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

#### Jumuiya ya Afrika Mashariki

44. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Februari 20-21, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 21 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika kwa njia ya mtandao. Katika Mkutano huo, Wakuu wa Nchi waliidhinisha lugha za Kiswahili na Kifaransa kutumika rasmi kwenye shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwezi Julai 20-20 hadi Aprili, 20-21 Tanzania ilitoa vyeti **Thelathini na saba Elfu, Mia Moja Kumi na Moja** vya uasili wa bidhaa kwa wafanyabishara wadogo wa Tanzania wanaofanya biashara katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vyeti hivyo, vimewasaidia wafanyabiashara kupata unafuu wa kodi kwa kutolipa ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazozalishwa nchini na zinazokidhi vigezo vya uasili wa bidhaa

Inaendelea Uk 14

Inatoka Uk 14

wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

*46.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika maandalizi ya Rasimu ya Katiba ya Fungamano la Kisiasa la Afrika Mashariki kama hatua ya mpito kuelekea Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Hadi kufikia mwezi Aprili 20-21, zoezi la kukusanya maoni na kutoa elimu kwa umma limefanyika katika nchi za Burundi na Uganda. Timu ya wataalam ya Jumuiya inayokusanya maoni kuhusiana na rasimu ya katiba hiyo itatembelea Tanzania mwezi Agosti 20-21. Maelezo ya kina yanapatikana kwenye **Aya ya 98 hadi 138** ya Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)**

*47.* ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Aprili 20-21, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Troika Mbili wa SADC uliofanyika jijini Maputo, Msumbiji. Katika Mkutano huo Nchi Wanachama ziliazimia kuendelea kushirikiana kuimarisha hali ya ulinzi na usalama kaskazini mwa Msumbiji hususan kwenye Jimbo la Cabo Delgado.

*48.* ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Machi 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa SADC uliofanyika kwa njia ya mtandao. Pamoja na masuala mengine, mkutano huo uliridhia kuongeza wigo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mikutano ya kisekta ya SADC. Maelezo ya kina yanapatikana kwenye **Aya ya 139 hadi 144** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**Umoja wa Afrika**

*49.* ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Februari 20-21, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 34 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo, uliridhia ombi la Tanzania la kujumuisha lugha ya Kiswahili na uanzishaji wa Kituo cha Urithi wa Afrika jijini Dar es Salaam katika programu ya kutekeleza kaulimbiu ya mwaka 20-21 inayosema **"Sanaa, Tamaduni na Urithi katika kufikia Azma ya Afrika Tuitakayo"**. Maamuzi hayo yamejumuishwa kwenye shughuli za programu hiyo zinazotekelezwa na Umoja wa Afrika katika mwaka 20-21. Maelezo ya kina yanapatikana kwenye **Aya ya 146 hadi 157** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**Ushirikiano wa Kimataifa**

*50.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Kikao cha 46 cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika mwezi Machi 20-21. Katika Kikao hicho, Tanzania ilipata fursa ya kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa haki za binadamu nchini ikiwa ni pamoja na hatua zilizofikiwa katika kutoa haki ya elimu, huduma za afya, maji safi na salama pamoja na nishati.

*51.* ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania pia ilitumia Kikao hicho kuielezea jumuiya ya kimataifa kuhusu Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba 20-20 ambao kwa mara ya kwanza katika historia ya Taifa letu uligharamiwa kwa fedha za ndani; na kuwa uchaguzi huo ulikuwa wa haki, huru na wazi, uliozingatia misingi ya demokrasia na utawala bora, na ulifanyika katika mazingira ya amani na utulivu. Hatua hizi, zimesaidia kujenga mtazamo chanya kwa jumuiya ya kimataifa kuhusu Taifa letu.

*52.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Kikao cha 75 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika kuanzia mwezi Septemba hadi Desemba 20-20. Tanzania ilitumia fursa hiyo kuieleza jumuiya ya kimataifa kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha huduma za kijamii na kutengeneza fursa za kiuchumi kwa kuimarisha miundombinu ya reli, barabara, maji, nishati, afya na elimu. Vilevile, Tanzania ilieleza kuhusu hatua zinazochukuliwa katika kupambana na rushwa na ubadhirifu wa mali za umma; kusimamia nidhamu kwenye utumishi wa umma; na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

*53.* ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina yanapatikana katika **Aya ya 160 hadi 164** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**4.3 Kufuatilia na Kusimamia Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na Hati za Makubaliano**

*54.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 20-20-21, Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano na kusimamia uwekaji saini Mikataba na Hati za Makubaliano mbalimbali ya Kimataifa kama ilivyoainishwa kwenye **Aya ya 165 hadi 166** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**4.4 KURATIBU MASUALA YA ITIFAKI, UWAKILISHI NA HUDUMA ZA KIKONSELI**

*55.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mahusiano ya Tanzania na nchi nyingine, Wizara imeendelea kuandaa na kuratibu ziara mbalimbali za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nje ya nchi. Aidha, Wizara imeratibu na kufanikisha ziara za Viongozi wa Mataifa mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa waliokuja Tanzania kwa ziara rasmi, kushiriki katika mikutano, makongamano na kutekeleza majukumu mbalimbali ya kitaifa. Maelezo ya kina yanapatikana kwenye **Aya ya 167 hadi 178** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**4.5 Uratibu wa Watanzania Wanaoishi Nje ya Nchi (Diaspora)**

*56.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu masuala yanayohusu jamii za Diaspora ili kuongeza mchango wao katika maendeleo ya Taifa. Kupitia jukumu hili, Tanzania imeendelea kunufaika na Diaspora ambapo kwa mujibu wa Benki Kuu ya Tanzania fedha zilizotumwa na Diaspora nchini kwa mwaka 20-20 zilikuwa ni Dola za Marekani milioni **Mia Moja Themanini na tisa nukta Moja Tatu**. Vilevile, katika kipindi hiki Diaspora wamenunua nyumba kupitia Shirika la Nyumba la Taifa zenye thamani ya **shilingi milioni mia nne ishirini na tatu nukta nane.**

**4.6 Elimu kwa Umma**

*57.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa za ajira, elimu, biashara, uwekezaji

na utalii zitokanazo n a uanachama wa Tanzania

Inaendelea Uk 15

Inatoka Uk 15

katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa pamoja na mahusiano na nchi nyingine. Fursa hizo hutangazwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari kama inavyoonekana kwenye **Aya ya 181** hadi **184** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**4.7 Utawala na Maendeleo ya Watumishi**

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi kwa lengo la kuboresha na kuimarisha utendaji wa kazi. Wizara ina jumla ya watumishi **mia nne hamsini na tano** wa kada mbalimbali. Kati yao watumishi **mia mbili ishirini na nane** wapo Makao Makuu ya Wizara na watumishi **mia mbili ishirini na saba** wapo kwenye Balozi za Tanzania. Katika kuimarisha utendaji kazi wa Wizara, masuala mbalimbali yanayohusu utawala na maendeleo ya watumishi yameendelea kusimamiwa kama ifuatavyo:

**4.8 Mafunzo na Upandishaji Vyeo**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ambapo jumla ya watumishi **mia mbili kumi na tisa** walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi. Watumishi wanane walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi **mia mbili kumi na moja** walihudhuria mafunzo ya muda mfupi. Aidha, jumla ya watumishi **mia mbili na nne** wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo. Taarifa ya kina ni kama inavyoonekana kwenye **Aya ya 187** hadi **190** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**4.9 Kuratibu na Kusimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara**

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 20-20-21, Wizara ilitengewa bajeti ya maendeleo ya **shilingi bilioni ishirini** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopo ndani na nje ya nchi. Wizara inaendelea kufuatilia Wizara ya Fedha na Mipango fedha za bajeti ya maendeleo zilizopangwa kwa Mwaka wa Fedha 20-20-21 mara baada ya kukamilisha nyaraka za miradi hiyo kama taratibu zinavyoelekeza.

**4.9.1 Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi Zilizo Chini ya Wizara**

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) kimeendelea kuendesha biashara ya mikutano; upangishaji wa nyumba na ofisi; na kutoa huduma ya afya kupitia hospitali inayomilikiwa na kituo hicho.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Diplomasia kinaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa Wizara/ Taasisi na Mashirika ya Serikali, mashirika na kampuni binafsi, balozi na watu binafsi; na kutoa mafunzo ya lugha saba za kigeni ambazo ni Kiarabu, Kifaransa, Kihispania, Kiingereza, Kichina, Kikorea na Kireno. Aidha, Chuo kimekamilisha mtaala wa mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa wageni.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini Katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM) ulifanya tathmini kuhusu utawala bora nchini na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa APRM nchini Tanzania. Taarifa hiyo imeangazia maeneo makuu manne ambayo ni: Demokrasia na Siasa; Usimamizi wa Uchumi; Utendaji wa Mashirika ya Biashara; na Maendeleo ya Jamii. Taarifa imeainisha mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha 2015 hadi 2019.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** kikao cha 30 cha Wakuu wa Nchi na Serikali zinazoshiriki Mpango wa APRM, kilichofanyika mwezi Machi 2021 wa njia ya mtandao kilimteua Mheshimiwa Balozi Ombeni Yohana Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu kuwa Mwenyekiti wa Jopo la Watu Mashuhuri wa APRM, Barani Afrika (The Panel of Eminent Persons). Napenda kutumia fursa hii kumpongeza kwa uteuzi huo. Tuna imani kuwa uzoefu wake wa muda mrefu na umahiri katika masuala ya diplomasia, utaendelea kuwa hazina na rasilimali ya kipekee kwa maslahi ya nchi yetu na Bara zima la Afrika. Taarifa ya kina ni kama ilivyobainishwa katika **Aya ya 191** hadi **205** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**5.0 SHUKRANI**

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kuzishukuru Balozi, Mashirika na Taasisi za Kikanda na Kimataifa na Washirika wa Maendeleo kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kufanikisha mipango mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali yetu.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nazishukuru nchi za Algeria, Australia, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Denmark, Ethiopia, Finland, Hispania, Hungary, Italia, Iran, Ireland, Indonesia, India, Israel, Jamhuri ya Korea, Japan, Kuwait, Malaysia, Malta, Marekani, Mexico, Misri, Morocco, New Zealand, Nigeria, Norway, Oman, Pakistan, Poland, Qatar, Romania, Saudi Arabia, Singapore, Sri Lanka, Sweden, Sudan, Thailand, Tunisia, Ubelgiji, Uganda, Ufaransa, Uingereza, Uholanzi, Ujerumani, Urusi, Uswisi, Uturuki, Ureno, Umoja wa Falme za Kiarabu, Venezuela na Viet Nam.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa shukrani pia kwa *ACBF;* AfDB; BADEA; DfID; EIB; EU; FAO; GiZ; IAEA; IFAD; ILO; IMF; IOM; JICA; KOICA; MASHAV; PAPU; OPCW; SIDA; UN; UNAIDS; USAID; UNCDF; UNCTAD; UNDP; UNEP; UNESCO; UNFPA; UNHCR; UNICEF; UNIDO; UNODO; UNWOMEN; UPU; WFP; WHO; na WWF. Vilevile, napenda kuwashukuru Abu Dhabi; *Association of European arliamentarians with Africa*; Benki ya Dunia; *Bill and Melinda Gates Foundation; Global Fund;* Investment Climate Facility for Africa; Khalifa Fund; Kuwait Fund; *Medecins Sans Frontieres; Red Cross*; *Trade Mark East Africa*; pamoja na Mifuko na Mashirika mbalimbali ya Misaada. Ni dhahiri kuwa ushirikiano wao umekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha malengo ya Serikali.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa moyo mkunjufu, napenda kuwashukuru watendaji na watumishi wa Wizara na Taasisi zake kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo. Kwa namna ya pekee, namshukuru Mhe. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (Mb), Naibu Waziri; Mhe. Balozi Joseph Edward Sokoine, Katibu Mkuu; Mhe. Balozi Fatma Mohammed Rajab, Naibu Katibu Mkuu; Waheshimiwa Mabalozi

Inaendelea Uk 16

Inatoka Uk 15

wa Tanzania; Wakuu wa Idara na Vitengo; Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara; na watumishi wote kwa kufanya kazi kwa umahiri, weledi na ufanisi.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda kuwashukuru Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi (Mb), aliyekuwa Waziri; Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb) na Mhe. William Tate Ole Nasha (Mb) waliokuwa Naibu Mawaziri; Mhe. Balozi Brig. Gen. Wilbert A. Ibuge aliyekuwa Katibu Mkuu na Dkt. Mwinyi Talib Haji aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu kwa mchango wao mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara katika Mwaka wa Fedha 20-20-21.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa nafasi ya kipekee kabisa, napenda kumshukuru mume wangu mpendwa Mhandisi Dkt. George Steven Mulamula; watoto wangu pamoja na familia yangu kwa ujumla kwa uvumilivu wao na kuwa karibu nami wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu ambayo wakati mwingine yananilazimu kuwa mbali nao kwa muda mrefu.

**6.0 MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 20-21-22, Wizara imeweka kipaumbele katika kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuendelea kutekeleza diplomasia ya uchumi;
ii. Kuendelea kuboresha na kuimarisha uhusiano na nchi nyingine, jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa;
iii. Kuendelea kulinda na kutetea misingi ya Taifa letu ndani na nje ya nchi;
iv. Kuendelea kushiriki kikamilifu katika kuimarisha utengamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika;
v. Kuendelea kushawishi na kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa nchi moja moja, jumuiya za kikanda na kimataifa; na
vi. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizopo chini ya Wizara.

72. ***Mheshimiwa Spika***, Majukumu mengine ni kama yalivyobainishwa katika **Aya ya 214** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**7.0 MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC)**

73. ***Mheshimiwa Spika,*** AICC imepanga kupanua huduma za afya kwa kukamilisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje la Hospitali ya AICC, ununuzi wa vifaa tiba; kujenga jengo la biashara jijini Arusha; na kukamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa Kituo cha mikutano kitakachoitwa Mount Kilimanjaro International Convention Centre (MK-ICC) jijini Arusha.

**Chuo cha Diplomasia**

74. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Diplomasia kimepanga kuendelea kutoa mafunzo ya mahusiano ya kimataifa; lugha ya Kiswahili kwa wageni; kuendelea kufanya tafiti katika maeneo ya mahusiano ya kimataifa na mbinu za kidiplomasia; kuendelea na ujenzi wa vyumba vya mihadhara kwa lengo la kuongeza udahili na mapato ya Chuo; na kuendelea kutoa ushauri na huduma za kitaalamu kwa Serikali na Taasisi zake.

**Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini Katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM)**

75. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021-22, APRM inatarajia kuendelea kufanya tathmini za utawala bora za mpango wa APRM ikiwa ni pamoja na kuhuisha mbinu za utafiti kwa kupitia upya hojaji ya APRM; kuandaa taarifa ya mwaka na kuweka mfumo madhubuti wa ufuatiliaji; na kuimarisha mawasiliano na utoaji taarifa kuhusu Mpango wa APRM.

**8.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

76. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 20-21-22, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha **shilingi bilioni mbili, milioni mia tano hamsini, laki nane sabini na tisa elfu** ikiwa ni mapato ya Serikali yatakayopatikana kutokana na vyanzo vilivyopo Makao Makuu ya Wizara na Balozi za Tanzania ambavyo ni pango la nyumba za Serikali zilizopo nje ya nchi na kuthibitisha nyaraka.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha 20-21-22, Wizara imetengewa bajeti ya kiasi cha **shilingi bilioni mia moja tisini na mbili, milioni mia mbili sitini na tano, laki nne thelathini na nane elfu**. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni mia moja sabini na nane, milioni mia saba sitini na tano, laki nne thelathini na nane elfu** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida zinazojumuisha **shilingi bilioni mia m o j a sitini na saba, milioni mia tisa thelathini na saba, laki mbili kumi na tisa elfu** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; **shilingi bilioni kumi, milioni mia nane ishirini na nane, laki mbili kumi na tisa elfu** kwa ajili ya Mishahara; na **shilingi bilioni kumi na tatu na milioni mia tano** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, **shilingi bilioni sita na milioni mia tano** ni kwa ajili ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa ofisi ya ubalozi na kitega uchumi ubalozi wa Tanzania Kinshasa, DRC; **shilingi bilioni tano** ni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na makazi ya balozi, ubalozi wa Tanzania Muscat, Oman; **shilingi bilioni moja** ni kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya Balozi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia; na **shilingi bilioni moja** ni kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Chuo cha Diplomasia.

**9.0 HITIMISHO**

79. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 20-21-22, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi bilioni mia moja tisini na mbili, milioni mia mbili sitini na tano, laki nne thelathini na nane elfu.** Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni mia moja sabini na nane, milioni mia saba sitini na tano, laki nne thelathini na nane elfu** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi bilioni kumi na tatu na milioni mia tano** ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia nafasi hii adhimu kukushukuru tena wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.



# Wizara sasa yatafuta makazi ya samaki wengi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Abdallah Kombo, amesema kuwa serikali imeandaa utaratibu wa kuyatambua maeneo yanayopatikana samaki kwa wingi.

Aliyasema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Viti Maalum, Khudhaima Mbarak Tahir, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi aliyetaka kujua utaratibu wa kuyatambua maeneo yanayopatikana samaki kwa wingi.

Waziri huyo alisema utaratibu huo tayari umeshaanza kupitia utekelezaji wa mradi wa SWIOFISH, lakini unahitaji muda, usahihi na umakini wa taarifa zaidi za kitaalamu na bado upo katika majaribio ya muda mrefu na unahitaji ushirikiano wa wataalamu wa uvuvi.

Alisema katika kufanikisha matokeo chanya ya utaratibu huo serikali hulazimika kutafuta njia za kuwapatia wavuvi vifaa vya aina ya GPS ili wakusanye taarifa za kimaeneo yanayokwenda katika shughuli zao za uvuvi wa kila siku.

"Ukiachia mfumo huu wa GPS, mpaka hivi sasa kuna njia mbili kubwa ambazo zinatumika kuyatambua maeneo yanayopatikana samaki kwa wingi," alisema.

Alibainisha kuwa njia ya kwanza ni kupitia ramani ambazo zinaonyesha mazingira ya bahari na afya yake ikijumuisha maeneo ya mikandaa (mangroves), majani ya bahari (seagrass) na matumbawe.

Alisema maeneo hayo hufanyiwa ukaguzi ili kubaini afya na ustawi pamoja na aina ya samaki wanaopatikana na wingi wake.

Alisema njia ya pili ni kwa kutumia elimu asilia na uzoefu kupitia wavuvi ambao wanatoa taarifa ya maeneo wanayopata samaki kwa wingi na aina ya samaki wanaopatikana katika maeneo hayo.



Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud (wapili kushoto), akisalimiana na viongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, akiwa katika ziara za kichama Mkoa wa Kaskazini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mamlaka Ndege Z'bar yaidai ATCL bil. 240/-

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Ndege (ATCL) linadaiwa Sh. bilioni 241 na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ikiwa ni ada ya utuaji na uegeshaji wa ndege za shirika hilo kwenye Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume Zanzibar.

Deni hilo ni la kuanzia Novemba 2007 hadi Desemba 2009.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Abdallah Kombo, alipojibu swali kwa niaba ya Waziri wa Wizara hiyo, Rahma Kassim Ali, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kilichofanyika Chukwani, Zanzibar.

Kombo ambaye ni Waziri wa Uchumi wa Buluu, alilazimika kutaja deni hilo baada ya kuulizwa swali na Mwakilishi wa Mfenesini, Machano Othman Said, katika kikao hicho.

Mbunge huyo alitaka kujua kiasi cha fedha ambacho mamlaka hiyo inalidai shirika hilo.

Waziri Kombo alisema mamlaka iliingia mkataba na ATCL kwa ajili ya utoaji wa huduma za utalii na uegeshaji wa ndege na ATCL ilitakiwa kulipa ada kutokana na huduma wanazopatiwa.

Alisema siku za mwanzo wa makubaliano hayo, shirika hilo lilikuwa likilipia huduma hizo kama inavyotakiwa lakini baadaye ATCL imeshindwa kulipa na kusababisha kulimbikizwa kwa deni hilo. Alisema deni hilo ni la muda mrefu na kwamba Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ina mpango wa kulipeleka suala hilo katika kamati inayoshughulikia masuala ya Muungano kwa kulipatia ufumbuzi.

# ACT yasisitiza wanachama kitambulisho cha Mzanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo Zanzibar, Juma Duni Haji, amewahimiza wafuasi wa chama hicho ambao hawajapata kitambulisho cha Mzanzibar mkaazi kufuatilia ili kupata haki yao hiyo ya kikatiba.

Aliyasema hayo kwa nyakati tofauti wakati wa ziara ya kumtambulisha mjumbe wa kamati kuu ya chama hicho na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, kwa viongozi wa mikoa, majimbo na matawi Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema wapo vijana wengi ambao tayari wamefikia umri wa miaka 18 ambao kwa mujibu wa katiba ni lazima wapatiwe kitambulisho hicho lakini takwimu zinaonyesha walio wengi bado hawajapatiwa.

Alisema kama vijana hao hawajafanya taratibu za kuomba kitambulisho hicho, watakuwa wamejikosesha haki ya kikatiba katika nchi yao.

"Kama mtu hana kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi hawezi kupata chochote, hasa ajira katika visiwa vya Zanzibar," alisema.

Kiongozi huyo alisema wananchi walikuwa wakipata tabu katika kupata kitambulisho hicho, lakini Mungu ameleta mabadiliko ya utawala na waziri husika ametangaza kabisa kuwa hakuna sababu ya mtu kunyimwa kitambulisho.

Aliwataka wananchi wasisubiri kipindi cha uchaguzi kufuatilia kitambulisho hicho na badala yake wafuatilie sasa.

Mjumbe wa Kamati Kuu na Makamu wa kwanza wa Rais Zanzibar, Masoud, alisema kutokana na umuhimu wa kitambulisho hicho ni busara kwenda kutafuta kitambulisho hicho.

Alisema kama vijana wa chama hicho hawatakuwa na vitambulisho itakuwa vigumu kupiga kura katika uchaguzi mkuu hali ambayo haitakuwa jambo rahisi kushinda katika uchaguzi huo.

**Kiongozi huyo alisema wananchi walikuwa wakipata tabu katika kupata kitambulisho hicho, lakini Mungu ameleta mabadiliko ya utawala na waziri husika ametangaza kabisa kuwa hakuna sababu ya mtu kunyimwa kitambulisho.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa***
***Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie 0782253676***

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANDERSON AGAEL MOLLEL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0542/0091/2017** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **OLDADAI** mwaka **2017,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**Polisi taarifa DAR/OST/RB/276509/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**RICHARD C. MWITA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0377/0660** kilichotolewa na **LUGALO J.W.T.Z CENTER** mwaka 2008. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: DAR/KIJ/R-B/276124/2021.

## KUPOTEA KWA CHETI



**STAMILI W. MAYOYO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1771/0044** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **VUMILIA** mwaka 2017,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DOD/DOD/RB/600215/2020**

## KUPOTEA KWA CHETI



**AMEDIUS WILISON** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0917/0020** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **IHEMBE SEKONDARI** mwaka **2014.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **CD/IR/RB/1709/2019.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**KUMBUSHO KIKOMBE** anatangaza kupotelewa na vyeti. Cheti cha kidato cha nne chenye Index **No.S0515-0045** kilichotolewa na Ilula secondary mwaka 2004. Cheti cha kidato cha sita chenye Index **No. S0413-0571** kilichotolewa na Kibiti secondary mwaka 2007. Cheti cha kidato cha sita chenye Index **No. P0368-0530** kilichotolewa na Imboru secondary Mwaka 2013. Cheti cha chuo chenye namba **M.BSCED0000299** kilichotolewa na University of Dar es Salaam mwaka 2016. Transcript ya chuo yenye Registration **No: 2013-04-05768** iliyotolewa na University of Dar es Salaam mwaka 2016. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **MAN/BAB/RB/274324/2021.**

## TANGAZO LA UKUMBI

**UKUMBI WA HARUSI NI BURE**
PR COMPLEX ILIYOPO SINZA BARABARA YA SHEKILANGO KARIBU NA HOSPITAL YA PALESTINA INATOA 'OFFER'YA UKUMBI BURE KUANZIA WATU 600 NA KUENDELEA KUNA STANDBY GENERATOR NA FULL 'AC' MAPAMBO.CHAKULA ,VITI,MEZA,MC NA MZIKI NI JUU YAKO.
VINYWAJI VINAPATIKANA UKUMBINI KWA BEI NAFUU.
KARIBUNI SANA.

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**




**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Tanzania kuzalisha na kuuza mbegu bora nje

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amesema serikali imejizatiti kufikia mwaka 2025, Tanzania itakuwa mzalishaji na muuzaji wa mbegu bora nje ya nchi.

Amesema hatua hiyo itaongeza tija na uzalishaji sambamba na kukuza pato la taifa.

Akizungumza baada ya kukitembelea kiwanda cha kuzalisha mbegu bora cha Seed Co Tanzania Limited, Prof. Mkenda alipongeza juhudi na kazi kubwa zinazofanywa na kiwanda hicho na kukitaka kuendelea na utafiti zaidi ili kuja na mbegu bora zaidi ambazo zitauzwa hata katika masoko ya nje na zitakazoongeza tija katika sekta ya kilimo.

"Kwa namna ya kipekee niwapongeze kwa kazi nzuri mnayofanya na nachukua fursa hii kuwaomba mjikite kwenye utafiti zaidi kwa kuwa hapa mna maabara nzuri ambayo mkiitumia vyema kwenye utafiti wenu mtakuja na matokeo chanya yatakayowezesha upatikanaji wa mbegu bora na nyingi zaidi zitakazosaidia maendeleo na ustawi wa sekta ya kilimo," alisema Prof. Mkenda.

Amesema lengo kubwa la wizara yake ni kuhakikisha sekta ya kilimo inajitegemea zaidi na hasa kuwa na mbegu bora ambazo zitaongeza tija na uzalishaji kwa wakulima waweze kupata mazao bora na yenye ushindani kwenye masoko ya ndani na nje.

Aidha, Waziri Mkenda alizitaka taasisi zingine kama TARI, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kuendelea na utafiti zaidi wa mbegu ili kusaidia kupata mbegu bora na zenye tija kwa wakulima.



Halmashauri ya Jiji la Mwanza, ikiwa imeyafunga maduka ya mfanyabiashara Christopher Tarimo jana, aliyeingia mkataba nayo wa kuyajenga katika Shule ya Sekondari Pamba jijini humo, licha ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kufanya ukaguzi wa kitega uchumi hicho na kuagiza jiji hilo lipate asilimia 40 ya mapato hakutekeleza agizo hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Stanbic kuwaunga mkono wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania imezindua awamu ya pili ya shindano la ujasiriamali linaloitwa, 'Stanbic Entrepreneurship Challenge' kwa lengo la kuwahamasisha na kuwaunga mkono Watanzania wenye ndoto za mafanikio.

Kampeni hii inaanza Mei 31, 2021 ambapo washindani 10 bora watajinyakulia shilingi milioni 5 za kitanzania kwa kila moja. Aidha, sehemu ya kwanza ya shindano hili ilizinduliwa Mei mwaka 2020 wakati ambao benki ilikuwa ikiadhimisha miaka 25 ya uwapo wake nchini Tanzania.

Mwaka huu shindano la 'Stanbic Entrepreneurship challenge' litalenga wajasiriamali wanaofanya kazi kwa bidii ili kufikia malengo yao kupitia miradi ambayo ina manufaa kwenye jamii, katika sekta za elimu, afya, mazingira, teknolojia pamoja na chakula na uzalishaji. Miongoni mwa vigezo vya ushiriki ni; washiriki lazima wawe ni wakazi wa mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Mwanza, Kilimanjaro na Dodoma. Masharti na maelekezo yote ya shindano hili yanapatikana kwenye tovuti na kurasa za mitandao ya kijamii ya benki ya Stanbic.

"Tunafurahia kutoa mchango wetu ili kuhamasisha ukuaji wa biashara ndogo na za kati, ambazo zina mchango muhimu kwenye uchumi wetu. Mara nyingi wajasiriamali wamekuwa wakileta mabadiliko na kuonyesha ubunifu ili kuleta maendeleo katika jamii zao," alisema Mkuu wa Masoko wa Benki ya Stanbic Tanzania, Desideria Mwegelo.

"Tumejidhatiti kutoa vitendea kazi sahihi kwa Watanzania wenye ndoto ili wafikie malengo yao ya kibiashara kupitia huduma zetu suluhishi kama vile Biashara Direct, pamoja na kampeni kama hii ya 'Stanbic Entrepreneurship Challenge." aliongeza.

# Urusi, Tanzania kushirikiana utunzaji mazingira

**Na Gwamaka Alipipi**

TANZANIA na Urusi zinatarajia kushirikiana katika kuanzisha, kukuza miradi ya mazingira ili kufikia kiwango cha kimataifa.

Mkuu wa Shirika na mwanachama wa Jumuiya ya Kijiografia ya Urusi, Yuri Korobov, alisema ushirikiano huo utajikita katika kudhibiti matukio ya ukataji misitu ya asili.

Korobov alisema: "Kwanza, tumejipanga kufanya kazi katika miradi ya mazingira. Hii ni kati ya Urusi na Tanzania, tatizo la ukataji miti hovyo ni baya. Kuna baadhi ya watu wamekuwa wakikata misitu ya asili iliyoenea kwenye maeneo mbalimbali".

Aliongeza: "Tanzania inakabiliwa na matatizo kadhaa ya mazingira, hiyo imekuwa ikiathiri maendeleo ya mazingira kwa kiasi kikubwa. Tatizo kubwa linaloikabili Tanzania ni uharibifu wa ardhi, uchafuzi wa mazingira, kukosa maji safi katika baadhi ya maeneo ya mjini na vijijini na upoteaji wa wanyamapori."

Alisema Jumuiya ya Urafiki ya Urusi inajipanga kufanya kazi na mashirika kama Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ambalo lina jukumu la kuishauri serikali juu ya mambo yote yanayohusiana na mazingira.

Korobov alisema pia wataangalia changamoto zingine ambazo zimekuwa kikwazo katika kuathiri mazingira Tanzania, kuangalia migodi iliyotelekezwa, ambayo haihifadhiwi vizuri baada ya kuchimba madini, ikitoa gesi hatari za kemikali ambazo husababisha uharibifu wa udongo, pamoja na ukataji miti kwa wingi

"Shida zote hapo juu zinaweza kupunguzwa kwa gharama ya teknolojia zilizopo nchini Urusi. Ndiyo sababu tumepanga kufanya mafunzo ya pamoja na kubadilishana wataalamu wanamazingira, wahandisi, wakemia na wanaojitolea," alisema Korobov.

Jumuiya ya Urafiki ya Urusi na Tanzania zinatarajiwa kutia saini makubaliano yao ya kwanza na Jumuiya ya Urafiki ya Tanzania mwishoni Juni, mwaka huu.

Aliongeza, wamepanga kutekeleza miradi mingine kadhaa, ikiwamo uundaji wa jukwaa la ushirikiano wa kiuchumi kati ya biashara ya Tanzania na Urusi lenye kaulimbiu ya kuvutia uwekezaji wa pande zote, utayarishaji wa mipango ya elimu kwa wanafunzi na vijana wa Urusi na Tanzania.

# ARSENAL YATAJIWA BEI YA ODEGAARD



**MADRID,** Hispania

KAMA Arsenal watataka kumsajili kiungo, Martin Odegaard, ambaye msimu huu alicheza kwa mkopo hapo kwao akitokea Real Madrid, watalazimika kutoa Euro milioni 60, imeelezwa.

Odegaard alisajiliwa na Real Madrid Januari 2015 akiwa miongoni mwa wachezaji vijana bora Ulaya, wakati huo akiwa na umri wa miaka 16 tu.

Katika hatua zake za ukuaji wake, Odegaard amepitia timu nyingi kwa mkopo.

Odegaard alitolewa kwa mkopo misimu ya 2018/2019 na 2019/2020 kwenda timu Vitesse Arhem na Real Sociedad ambapo alifaulu kwenye LaLiga na kuibuka kuwa miongoni mwa wachezaji bora vijana msimu huo, baada ya hapo akaitwa Real Madrid, ambapo alijumuishwa kwenye kikosi cha msimu wa 2020/2021.

Uwapo wa watu kama Toni Kroos na Luka Modric, ulimpa nafasi finyu Odegaard na baada ya hapo akaelekea kwa mkopo Arsenal ambapo tangu ajiunge nao Januari, amefunga mabao mawili na pasi mbili kwenye mechi 20.

Amekuwa sehemu muhimu katika kikosi cha Arsenal na 'Washikabunduki' hao wanatamani kumsajili moja kwa moja na Madrid wanataka Euro milioni 60 mezani ili wamuachie.

Baada ya kumalizika kwa msimu wa Ligi Kuu England, mchezaji huyo atarudi tena Madrid ambapo ataendelea kusalia hapo ila wanaweza kumuuza.

# Anceloti kumrithi Zidane Real

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imekuwa na mawasiliano na Carlo Ancelotti ili kuchukua nafasi ya Zinedine Zidane, kwa mujibu wa Calciomercato.

Real Madrid inajua kwamba, Ancelotti anaweza kufanya vizuri zaidi kuisaidia klabu hiyo, kama ambavyo alishawahi kufanya hivyo hapo nyuma.

Kocha huyo mkongwe raia wa Italia, aliwaongoza 'Los Blancos' hao kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2014.

Ancelotti ambaye kwa sasa anainoa Everton, awali aliinoa Real Madrid kuanzia mwaka 2013 hadi 15, akishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya na lile la Klabu Bingwa Dunia mwaka 2014.

Cadena SER, imeripoti kuwa Rais Florentino Perez, amefikia makubaliano na Ancelotti na Everton imeanza kutafuta mtu wa kurithi mikoba yake mara tu atakapoondoka.

Majina kadhaa yamekuwa yakitajwa kuhusishwa na kazi ya kuchukua mikoba pale katika dimba la Bernabeu, yakiwamo Mauricio Pochettino, Antonio Conte, Raul na Xabi Alonso.






# *Copa America 2021 sasa kufanyika Brazil*

**RIO DE JAINERO,** Brazil

SHIRIKISHO la Soka la Bara la Amerika Kusini (CONMEBOL), limethibitisha kwamba, mashindano ya Copa America 2021, yatafanyika kama yalivyopanga, huku sasa Brazil ikipewa jukumu la kuandaa.

Michuano hiyo ilipangwa kufanyika mwaka 2020, lakini iliahirishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona na awali ilipangwa kufanyika kwa ushirikiano wa nchi mbili Colombia na Argentina.

Hata hivyo, Colombia ikaondolewa baada ya wananchi kuandamana nchini humo, huku Argentina kwa sasa ikikabiliwa na ongezeko kubwa la virusi vya corona na hivyo nao wameondolewa.

CONMEBOL ilikutana Jumatatu kutangaza mwandaaji mpya wa mashindano hayo na nafasi hiyo ikaangukia kwa Brazil, ambayo ililitwaa taji hilo mwaka 2019 katika ardhi ya nyumbani kwake.

Katika ujumbe uliowekwa kwenye ukurasa wa Twitter wa shirikisho hilo ulisomeka: "Copa America 2021 itafanyika nchini Brazil!

"Mashindano yataanza na kumalizika kwa tarehe zilizotajwa. Viwanja na tarehe za mechi vitatajwa na CONMEBOL saa chache zijazo."

Michuano hiyo itaanza Juni 13 na kumalizika Julai 10, ingawa taarifa zaidi kuhusiana na mashindano hayo hazijatolewa.

# HAZARD: SINA MPANGO KUONDOKA MADRID




**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard amesisitiza hana mpango wa kuondoka Real Madrid licha ya kutokuwa kwenye kiwango bora tangu atue hapo kutoka Chelsea, na anataka kupambania nafasi yake.

Hazard alisaini mkataba wa miaka mitano na Madrid mwaka 2019, akijiunga kwa ada iliyoripotiwa kuwa Euro milioni 100 baada ya misimu saba yenye mafanikio kule Stamford Bridge.

Hata hivyo, majeraha ya mara kwa mara yamemfanya nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji kuwa kwenye wakati mgumu na kushindwa kung'ara huko Hispania na akianza katika mechi 21 tu za Ligi Kuu Hispania, kwa kipindi cha miezi miwili.

Hazard ameanza katika kikosi cha kwanza katika mechi 11 msimu huu wa 2020-21 kwenye mashindano yote, akifunga mara nne na kutoa pasi za mwisho mbili.

Imeripotiwa kwamba, Madrid inajiandaa kumuuza Hazard na ipo tayari kusikiliza ofa ya kuanzia Euro milioni 50 kwa dirisha lijalo la usajili, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, hana mpango wa kukata tamaa hapo Santiago Bernabeu.

"Bado nina miaka mitatu na Real Madrid. Naipenda klabu. Nawapenda wachezaji. Nitajitoa kwa kila kitu msimu ujao kwa klabu hiyo.

"Najiona mwenyewe kwamba siwezi kuondoka Real Madrid sasa," alisema Jumatatu akiwaambia waandishi wa habari.

## Zidane atoa sababu kuondoka Madrid



**MADRID,** Hispania

KOCHA Zinedine Zidane, ameweka wazi sababu iliyomfanya kuondoka ndani ya Real Madrid huku akidai kubwa zaidi ni viongozi kukosa imani naye.

"Nimeamua kuondoka Madrid kwa kuwa ni wazi viongozi na vyombo vya habari havikuwa na imani na mimi," alisema Zidane akinukuliwa na Marca.

"Mara zote kupitia vyombo vya habari utasikia vitisho kuwa nisiposhinda mchezo nitafutwa kazi, nayasikia hayo na hata jumbe za siri za viongozi zinavuja kwenda kwa wanahabari.

"Bahati nzuri kila jambo likitokea wachezaji wangu walikuwa upande wangu na walifanya kila kitu uwanjani kwa ajili yangu, kwa kuwa wananiamini nami nawaamini.

"Sisemi kuwa mimi ni bora sana, lakini ninapopewa kazi nafanya kile nilichotumwa kwa nguvu yangu na uwezo wangu na mara zote nimetimiza."

Zidane ametamka maneno hayo kwa mara ya kwanza tangu aondoke Real Madrid, baada ya kumaliza msimu akiwa hana taji hata moja.

## *Conte atajwa Spurs, Madrid*

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte ameripotiwa kuwa katika mazungumzo na Real Madrid na Tottenham Hotspur, na anaweza kuungana tena na Mkurugenzi wa zamani wa Juventus, Fabio Paratici, pale Spurs.

Kocha huyo kwa sasa yupo huru, baada ya kuvunja mkataba wake na Inter Milan kwa makubaliano, baada ya kushinda taji la Serie A. Kuna kifungu katika makubaliano ya awali ambacho kinaainisha kuwa hawezi kufanya kazi kwa klabu nyingine ya Italia kwa msimu ujao, kwa hiyo anataka kuhamia nje ya nchi hiyo.

Kwa mujibu wa Sportitalia, Conte ameanza mazungumzo na Real Madrid na kuwasilisha maombi yake kwa bosi Florentino Perez.

Lakini, Diario AS imeripoti kuwa Perez hajafurahishwa na mtazamo wa namna Conte anavyowasilisha ofa zake.

Ripoti hiyo hiyo inasema kuwa kocha huyu pia yuko kwenye mazungumzo na Tottenham.

Kuna jambo la ziada kwa pendekezo la Spurs, kwani Conte angeweza kuungana tena na Mkurugenzi Paratici.

Paratici na Beppe Marotta walimleta Conte pale Juventus mwaka 2010, akianza vema kwa kushinda misimu tisa.

Tangu wakati huo, Marotta amehamia Inter na Paratici hakupewa nyongeza ya mkataba pale Juventus.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AGUERO RASMI ASAINI MIAKA MIWILI BARCA

## Aacha rekodi kibao Manchester City huku pia akimpiku Rooney kwa...

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imekamilisha usajili wa gwiji wa Manchester City, Sergio Aguero akiwa mchezaji huru.

**Straika huyo mwenye umri wa miaka 32, alifanyiwa vipimo vya afya Jumatatu nchini Hispania, ikiwa ni siku mbili tu baada ya kuichezea mechi ya mwisho City kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo walifungwa bao 1-0 na Chelsea.**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina, ambaye atacheza sambamba na rafiki yake wa utotoni, Lionel Messi hapo kwenye dimba la Camp Nou, amesaini mkataba wa miaka miwili huku kukiwa na kipengele cha mkataba wa bonasi ya Euro milioni 100.

Atajiunga rasmi na timu hiyo kuanzia Julai Mosi, mwaka huu wakati ule wa Man City utakapomalizika mwishoni mwa mwezi huu.

"Kila mmoja wetu hapa Manchester City angependa kuchukua nafasi hii kumshukuru Sergio kwa mchango wake alioutoa katika mafanikio yetu ya kipindi cha muongo mmoja na tunamtakia kila la heri katika maisha yake mapya ya soka," ilisomeka taarifa ya Man City ambao ni mabingwa wa Ligi Kuu England.

Aguero alitumia miaka mitano akicheza kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, akiwa na Atletico Madrid hadi mwaka 2011, wakati alipohamia kule City kwa ada ya pauni milioni 35.

Alifunga mabao 260 katika mechi 389 ambapo ameweka rekodi ya ufungaji wa muda wote hapo Manchester.

Aguero ambaye alitwaa taji la kwanza la Ligi Kuu England akiwa na City msimu wa 2011-12, akifunga bao la dakika za majeruhi dhidi ya QPR kwenye mchezo wa mwisho wa Ligi Kuu, ameshinda mara tano taji la EPL.

Ameshinda mara sita taji la EFL na FA na msimu wa 2018-19, alikuwa sehemu ya kikosi cha kocha Pep Guardiola kilishoshinda mataji matatu.

Aguero alifunga mara mbili kwenye mchezo wake wa mwisho wa Ligi Kuu kuichezea City wakati ikishinda mabao 5-0 dhidi ya Everton wiki iliyopita.

Mabao hayo yalimfanya kufikisha 184 kwenye Ligi Kuu England na akishika nafasi ya nne kwa kuwa mfungaji wa wakati wote na akiivunja rekodi ya Wayne Rooney ya kufunga mabao mengi katika mashindano hayo.

## ZISIKUPITE

### TOMORI KUBAKI MILAN

FIKAYO Tomori anapanga kubakia AC Milan kwa mkataba wa kudumu wa miaka mitano. Chelsea watalipwa Euro milioni 28 kwa ajili ya kumwachia mchezaji wake huyo ambaye alikuwa akicheza kwa mkopo kule Milan. ***(Sky Sport)***

### EVERTON YAMTAKA PEDRO

KLABU ya Everton inataka kumrudisha Pedro kwenye Ligi Kuu England, lakini bado hawajatoa ofa rasmi kwa AS Roma kuhusu nyota huyo wa zamani wa Chelsea. ***(Calciomercato)***

### SARRI KUTUA LAZIO

KOCHA wa zamani wa Juventus, Maurizio Sarri, anapewa nafasi kubwa zaidi ya kuchukua mikoba ya kuinoa Lazio. ***(Calciomercato)***

### CHELSEA YAKOMAA NA LUKAKU

CHELSEA ipo tayari kumsajili tena mshambuliaji wa Inter Milan, Rumelu Lukaku, 28, msimu huu wa majira ya joto huku klabu hiyo ya Italia ikiwa imejiandaa kusikiliza ofa kwa ajili ya Mbelgiji huyo. ***(Mail)***

### WATFORD WAMTAKA NKETIAH

KLABU ya Watford inataka kumsajili mshambuliaji, Eddie Nketiah, lakini Arsenal wanataka pauni milioni 15 kwa ajili ya Muingereza huyo, ambaye amebakisha mwaka mmoja kwenye mkataba wake na Arsenal. ***(Sun)***

### SANCHO AKARIBIA UNITED

MANCHESTER United wamekubaliana masharti binafsi na Jadon Sancho, 21, lakini bado hawajatoa ofa rasmi kwa winga huyo wa Borussia Dortmund na England. ***(Sport 1, via Star)***

### TUCHEL KUFUNGWA CHELSEA

THOMAS Tuchel yuko karibuni kusaini mkataba mpya baada ya kuiongoza Chelsea kunyakua taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku Mjerumani huyo akitarajiwa kupatiwa mkataba hadi mwaka 2023. ***(Guardian)***

### CONTE KUTUA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur wanafanyia kazi uteuzi wa Antonio Conte kama kocha mpya sambamba na Mkurugenzi wa Michezo wa zamani wa Juventus, Fabio Paratici kama mkurugenzi wa michezo. ***(Sport Italia, via Express)***

### RIDIGER AWANIWA SPURS

TOTTENHAM pia inapanga uhamisho wa kushtukiza wa mlinzi wa Chelsea, Antonia Rudiger, 28, ingawa wanaweza kukutana na ushindani kutoka Paris St-Germain. ***(Mirror)***

### NIGUEZ AITAKA UNITED

KIUNGO wa Atletico Madrid, Saul Niguez, 26, atashinikiza kuhamia Manchester United mbele ya Juventus au Paris St-Germain katika dirisha la usajili la majira ya joto. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

## Coastal: Msitarajie tutashuka daraja

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na kuwa nafasi ya tatu kutoka chini huku ikiwa imebakisha mechi tano imalize ligi, klabu ya Coastal Union imesema kuwa imejipanga kupambana ili kutoshuka daraja.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mgunda, amesema kwa sasa wamejipanga kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye mechi zilizobaki na wana uhakika kuwa watafanikiwa na suala la kushuka daraja halipo.

Alisema ameshawaandaa vijana wake kwa mechi zilizobaki ambazo ni za kufa au kupona kwa sababu kilichobaki sasa si mambo ya kufikirika, bali ni uhalisia.

Kwa sasa Coastal ipo nafasi ya 16, ikiwa na pointi 33 kwa mechi 29 ambazo imecheza na imebakiza mechi dhidi ya Kagera Sugar, Mwadui, Simba, Prisons na Mbeya City.

## Mkwasa apania kuishangaza Simba

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI kesho wakishuka katika Uwanja wa CCM Kirumba kuikaribisha Simba kwenye mechi yao ya kiporo ya Ligi Kuu Bara, Benchi la Ufundi la Klabu ya Ruvu Shooting limesema, limejipanga vizuri kuwakabili mabingwa watetezi hao na linatarajia kuishangaza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Boniface Mkwasa, alisema hana wasiwasi na mchezo huo licha ya kuwa wanakwenda kukutana na timu yenye wachezaji bora.

"Tumejipanga vizuri kukutana na Simba kesho, wachezaji wote wapo vizuri kwa ajili ya mchezo huo, tunaomba mashabiki pamoja na wadau wetu waendelee kuiunga mkono timu yetu," alisema Mkwasa.

Kocha huyo alisema mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani kutokana na maandalizi yaliyofanywa na timu zote mbili, lakini ana matumaini ya kupata matokeo.

# MINZIRO HATARAJII KUONA AKITIMULIWA GEITA GOLD

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Geita Gold ambayo imepanda Ligi Kuu hivi karibuni na Jumapili iliyopita kutwaa ubingwa wa Ligi Daraja la Kwanza, Felix Minziro, amesema anaamini kuwa atasalia kwenye kikosi hicho kwa sababu ya mkataba mzuri alionao.

Akizungumza baada ya timu yake hiyo kuifunga Mbeya Kwanza bao 1-0 kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na kutawazwa Mabingwa wa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara, Minziro alisema ameshafanya mazungumzo na uongozi wa Geita Gold na kukubaliana kuwa atasalia kwenye kikosi hicho kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Huko nyuma tatizo mikataba inakuwa haiko vizuri, lakini mkataba wa Geita Gold uko vizuri tu na tayari tumeshafanya maongezi nao wamenihakikishia kuwa nitaendelea kuwapo," alisema Minziro.

**Kocha huyo alisema hayo kutokana na rekodi yake ya kutupiwa virago kila anapoipandisha timu Ligi Kuu.**

Msimu wa 2016/17, aliichukua timu ya Singida United ikicheza Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara na kufanikiwa kuipandisha Ligi Kuu, ikianza rasmi kucheza msimu wa 2017/18. Hata hivyo, timu hiyo ilishuka msimu wa 2019/20, wakati yeye akiwa ameshatimuliwa.

Minziro pia aliitwaa timu ya KMC na kuiongoza kucheza Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara msimu wa 2017/18, ikafanikiwa kukwea Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2018/19 na hadi leo bado ipo, lakini akiwa ameshafungashiwa virago.

Mara zote hizo, Minziro alikuwa akiondolewa tu timu hizo zinapopanda Ligi Kuu, hivyo kukawa na wasiwasi kwamba huenda Geita Gold nayo ikafanya hivyo.

Mbali na kuipandisha Ligi Kuu, Minziro pia Jumapili, alitangazwa kuwa kocha bora wa ligi hiyo. Geita Gold iliyopanda kutoka Kundi B, ilishinda bao hilo kwenye fainali iliyochezwa dakika 120 dhidi ya Mbeya Kwanza ambayo ilikuwa ya kwanza kupanda msimu huu, ikitokea Kundi A.

**WASHA MDUNDO...**




Meneja Mwandamizi wa Chapa ya Coca-Cola Tanzania, Kabula Nshimo (kushoto), akimkabidhi zawadi nahodha wa timu ya Taifa, 'Taifa Stars' na mshambuliaji wa Klabu ya Fenerbahce ya Ligi Kuu Uturuki, Mbwana Samatta wakati alipotembelea kiwanda cha kampuni hiyo kujionea mchakato mzima wa utengenezaji wa kinywaji cha Coca-Cola. Samatta ambaye ni mwakilishi wa Coca-Cola Tanzania wa kuitangaza chapa ya kampuni hiyo katika kampeni zake ili kuwahamasisha Watanzania kufikia ndoto zao, alishirika kwenye uzinduzi wa Kampeni ya 'WASHA MDUNDO.' **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Simba yafunika bonasi SportPesa, yazoa milioni 450/-*

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Simba imeweka rekodi ya kubeba tuzo tano kutoka Kampuni ya Michezo ya Burudani ya SportPesa baada ya kufanya vizuri katika mashindano matatu tofauti iliyoshiriki huku ikiongoza kwa kuchota bonasi ya Sh. milioni 450 ndani ya miaka minne.

Kiasi hicho cha fedha kinakuja baada ya timu hiyo kufanikiwa kufuzu hatua ya robo Fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika mara mbili kabla ya kutolewa na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini msimu huu.

Baada ya kufanikiwa kufuzu hatua ya robo fainali, wiki iliyopita SportPesa iliwapa bonasi ya Sh. milioni 50 kutokana na hatua waliyofikia katika michuano hiyo mikubwa.

Bonasi hiyo ni sehemu ya udhamini ambayo ipo katika mkataba wa udhamini tangu SportPesa iliposaini mkataba wa kuidhamini mwaka 2017 ikizihusisha Simba na Yanga.

Simba tangu iingie udhamini na SportPesa, imefanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara mara tatu mfululizo msimu wa 2017/2018, 2018/ 2019 na 2019/ 2020 na kujizolea kitita jumla ya Sh. milioni 300 kwa kila msimu huku ikilamba pia Sh. milioni 100 baada ya kufika Fainali ya Kombe la Kagame msimu wa 2017 kabla ya kupata bonasi nyingine ya Sh. milioni 50 wiki iliyopita baada ya kufika hatua ya Robo Fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambazo zinaifanya jumla kuondoka na Sh. milioni 450.

Akizungumzia hatua hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas, aliipongeza Simba kwa hatua nzuri waliyofikia katika michuano hiyo mikubwa Afrika na mashindano mengine wanayoshiriki.

"Nawapongeza viongozi na wachezaji wa Simba kwa kuwapa heshima kubwa mashabiki wao kote nchini na kubwa zaidi ni heshima mliyotupa sisi kama wadhamini wenu wakuu kwa mafanikio makubwa na kupambana mpaka kufikia hatua hii.

"Tunachokifanya ni kutimiza moja ya ahadi tuliyotoa wakati tunasaini mkataba wa udhamini mwaka 2017 kuwa tutatoa bonasi ya Sh. milioni 50 endapo mojawapo ya timu tunazozidhamini zitafuzu hatua ya robo fainali kwenye michuano ya kimataifa," alisema.

# Michezo

Jumatano Juni 2, 2021

Nipashe




Aguero rasmi asaini miaka 2 Barca UKURASA 22

KATUTANGAZE...



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaru (kushoto), akizungumza na mchezaji wa Kimataifa wa Ufaransa anayeichezea Klabu ya Ligi Kuu England, Crystal Palace, Mamadou Sakho, walipokutana nje ya ukumbi wa Bunge jijini Dodoma baada ya ziara ya mchezaji huyo bungeni hapo jana, alitangazwa kuwa Balozi wa Hiari wa Utalii wa Tanzania. Katikati ni Mbunge wa Jimbo la Manonga, Seif Gulamali. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## CAS kumaliza utata Yanga, Morrison leo

**Na Mwandishi Wetu**

MBIVU mbichi ya sakata la Yanga na Bernard Morrison zinatarajiwa kujulikana leo kutoka Mahakama ya Usuluhishi ya Kimataifa ya Michezo (CAS), baada ya awali kutupilia mbali pingamizi la winga huyo Mghana, kutaka kesi iliyofunguliwa na klabu hiyo dhidi yake imalizikie nchini.

CAS imeamua shauri hilo ambalo Yanga inadai Morrison amesaini kwa wapinzani, Simba akiwa na mkataba na 'Wanajangwani' hao litasikilizwa leo.

Yanga imewataka mashabiki, wanachama na wapenzi wake kuwa watulivu wakisubiri uamuzi wa suala hilo kwa kuwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za uendeshaji wa mashauri katika mahakama hiyo klabu haitakiwa kuelezea mwenendo wa kesi mpaka itakapotolewa maamuzi.

"Klabu inapenda kuwatoa wasiwasi wanachama, wapenzi na mashabiki wake kwamba inaendelea kupambania haki zake mpaka haki itendeke, na klabu itawafahamisha maamuzi yatakayotolewa na mahakama hiyo," imeeleza taarifa ya Yanga.

# Gomes, Mkwasa vita vya kibabe

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

## ●●● Kila mmoja apania ushindi wakati zikishuka Kirumba kesho huku rekodi zikionyesha...

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wametua jijini Mwanza tayari kwa mechi yao dhidi ya Ruvu Shooting, itakayopigwa katika Uwanja wa CCM Kirumba kesho huku Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Didier Gomes, akisema wanachohitaji ni pointi tatu tu na si vinginevyo.

**Simba itashuka dimbanni kesho ikitaka kuendeleza kasi yake ya ushindi kwenye viporo vyake baada ya Jumamosi kutoka kuibabua Namungo FC mabao 3-1 katika mechi ya ligi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi.**

Hata hivyo, licha ya Ruvu Shooting kushuka dimbani ikiwa na jeraha bichi kutokana na kuadhibiwa mabao 3-1 na Kagera Sugar katika Uwanja wa Kaitaba Mjini Bukoba Mei 17, mwaka huu, ni wazi itakuwa na ari ya kutaka kuendelea kuitambia Simba kutokana na kuichapa bao 1-0 katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Tayari Kikosi cha Simba kimetua jijini Mwanza kwa ndege tangu jana mchana kikiwa na jeshi lake kamili kuelekea mechi hiyo ya kesho ambayo inatarajiwa kuwa ya kibabe na burudani ya kuvutia kutokana na timu zote kuwa na uwezo wa kuuchezea mpira.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Simba, Gomes, alisema kila mchezo kwao ni muhimu kushinda na anahitaji kuona wakiibuka na ushindi mbele ya Ruvu Shooting ili kufikia malengo yao jambo linalowafanya wawe na hesabu kali kila wanaposhuka uwanjani.

Alisema wana mechi nyingi za kucheza kwa sasa, hali ambayo inawalazimu kuongeza umakini na tayari hesabu zao wamezielekeza kuvuna pointi tatu dhidi ya Ruvu Shooting.

"Mechi ya kwanza tulipoteza mbele ya wapinzani wetu hao, sasa hatutaki kurudia makosa ya awali, utakuwa ni mchezo wa ushindani mkubwa na mgumu kwa sababu tunahitaji kuvuna pointi tatu kwao kama ambavyo nao wanahitaji.

"Kikubwa tunachohitaji ni ushindi tu katika mchezo huo, ila tunawaheshimu wapinzani wetu, hivyo tutaingia uwanjani kwa tahadhari kubwa ya kwenda kutafuta matokeo chanya," alisema Gomes.

Alisema ana matumaini makubwa na wachezaji wake kufanyia kazi yale anayowapa katika mazoezi na kuonyesha uwanjani kwa sababu amekuwa akiridhishwa na jinsi ambavyo nyota wake hao wanavyopambana katika kila mechi na kupata ushindi.

"Tunahitaji sana ushindi ili kufikia malengo yetu ya kutetea ubingwa, nina imani kubwa na vijana wangu kufanikisha kile ambacho mashabiki na Wanasimba wanakitarajia mwishoni mwa msimu huu," alisema Gomes.

Wakati Gomes akieleza hayo, Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Boniface Mkwasa, amesema hana wasiwasi na mchezo huo licha ya kuwa wanakwenda kukutana na timu yenye wachezaji bora.

"Tumejipanga vizuri kukutana na Simba kesho, wachezaji wote wapo vizuri kwa ajili ya mchezo huo, tunaomba mashabiki pamoja na wadau wetu waendelee kuiunga mkono timu yetu," alisema Mkwasa.

Simba ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 64 baada ya kushuka dimbani mara 26 wakati Yanga iliyocheza mechi 29, ikiwa na alama 61 katika nafasi ya pili, huku Ruvu Shooting iliyoshuka dimbani sawa na 'Wanajangwani' hao wakiwa katika nafasi ya 10 na pointi zao 37.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >